SERIKALI YA MAPINDUZI YA
ZANZIBAR

# SERA YA MAENDELEO YA VIJANA ZANZIBAR



2023

WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA
MICHEZO ZANZIBAR

DIBAJI vi
SHUKURANI viii
**SURA YA KWANZA** **1**
1.0 UTANGULIZI 1
1.1 Usuli 1
1.2 Upeo wa Sera 3
1.3 Uhusiano na Sera Nyingine za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa 3
**SURA YA PILI** **14**
2.0 HALI HALISI YA VIJANA ZANZIBAR 14
2.1 Vijana na Afya 14
2.2 Vijana na Uzalendo 15
2.3 Vijana na Utawala Bora 15
2.4 Vijana na Stadi za Maisha 16
2.5 Vijana na Ajira 16
2.6 Vijana na Elimu 17
2.7 Vijana na Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Amali na Ujasiriamali 18
2.8 Vijana na Teknolojia na Ubunifu 18
2.9 Vijana Wenye Ulemavu na Wenye Mahitaji Maalumu 19
2.10 Vijana na Mazingira 19
2.11 Ushiriki na Ushirikishwaji wa Vijana 20
2.12 Vijana na Usawa wa Kijinsia, Vita dhidi ya Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia 21
2.13 Vijana na Silka, Utamaduni na Sanaa 21
2.14 Vijana na Michezo 22
**SURA YA TATU** 23
3.0 DIRA, DHAMIRA, MALENGO MAKHUSUSI NA KANUNI ELEKEZI ZA SERA 23
3.2 Dira ya Sera 24

3.3 Dhamira ya Sera 24
3.4 Lengo Kuu la Sera 25
3.5 Malengo Mahususi 25
3.6 Kanuni Elekezi za Sera 26
**SURA YA NNE** **27**
4.0 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA 27
4.1 Hoja ya Sera: Vijana na Afya 27
4.1.1 Tamko la Sera: 27
4.1.2 Mikakati ya Sera 27
4.2 Hoja ya Sera: Vijana na Utawala Bora na Uzalendo 27
4.2.1 Tamko la Sera: 28
4.2.2 Mikakati ya Sera 28
4.3 Hoja ya Sera: Vijana Ajira na Uwezeshaji kiuchumi 28
4.3.1 Tamko la Sera: 29
4.3.2 Mikakati ya Sera: 29
4.4 Hoja ya Sera: Vijana na Elimu 29
4.4.1 Tamko la Sera: 30
4.4.2 Mikakati ya Sera: 30
4.5 Hoja ya Sera: Vijana na Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Amali na Ujasiriamali 30
4.5.1 Tamko la Sera: 31
4.5.2 Mikakati ya Sera: 31
4.6 Hoja ya Sera: Vijana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano 31
4.6.1 Tamko la Sera: 32
4.6.2 Mikakati ya Sera: 32
4.7 Hoja ya Sera: Vijana Wenye Ulemavu na Wenye Mahitaji Maalum 32
4.7.1 Tamko la Sera: 32
4.7.2 Mikakati ya Sera: 33

4.8 Hoja ya Sera: Vijana na Mazingira 33
4.8.1 Tamko la Sera: 33
4.8.2 Mikakati ya Sera: 33
4.9 Hoja ya Sera: Ushiriki na Ushirikishwaji wa Vijana 34
4.9.1 Tamko la Sera: 34
4.9.2 Mikakati ya Sera: 34
4.10 Hoja ya Sera:Vijana na mapambano dhidi ya ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia 35
4.10.1 Tamko la Sera: 35
4.10.2 Mikakati ya Sera 35
4.11 Hoja ya Sera: Vijana na Utamaduni na Sanaa 36
4.11.1 Tamko la Sera: 36
4.11.2 Mikakati ya Sera: 36
4.12 Hoja ya Sera: Vijana na Michezo 37
4.12.1 Tamko la Sera: 37
4.12.2 Mikakati ya Sera: 37
4.13 Hoja ya Sera: Vijana na Stadi za Maisha 38
4.13.1 Tamko la Sera: 38
4.13.2 Mikakati ya Sera: 38
**SURA YA TANO** 39
5.0 MFUMO WA KITAASISI, KISHERIA NA URATIBU WA SERA 39
5.2 Mfumo wa Kisheria 39
5.3 Majukumu na Wajibu wa Wadau katika utekelezaji wa Sera 39
5.3.1 Wizara Inayohusika na Masuala ya Maendeleo ya Vijana 39
5.3.2 Wizara inayohusika na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali 40
5.3.3 Wizara inayohusika na Elimu 40
5.3.4 Wizara inayohusika na Ajira, Kazi na Utumishi wa Umma 41
5.3.5 Wizara inayohusika na Habari na Mawasiliano 41
5.3.6 Wizara inayohusika na Utalii na Uchumi wa Buluu 41

5.3.7 Wizara inayohusika na Kilimo, Maliasili na Mifugo 42
5.3.8 Wizara inayohusika na Viwanda na Biashara 42
5.3.9 Wizara inayohusika na Fedha na Uwezeshaji kiuchumi 43
5.3.10 Wizara inayohusika na Sheria na Utawala Bora 43
5.3.11 Wizara inayohusika na Afya 44
5.3.12 Wizara inayohusika na Mazingira 44
5.3.13 Wizara inayohusika na Mila, Utamaduni na Sanaa 44
5.3.14 Wizara inayohusika na Michezo 44
5.3.15 Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa 45
5.3.16 Sekta Binafsi 45
5.3.18 Baraza la Vijana Zanzibar 46
5.3.19 Asasi za Kiraia 46
5.3.20 Asasi za Kidini 47
5.3.21 Vyombo vya Habari 47
5.3.22 Jamii na Wazazi 47
**SURA YA SITA** 49
6.0 URATIBU, UFUATILIAJI, TATHMINI NA MAPITIO YA SERA 49
*6.1 Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini* 49
*6.2 Mapitio ya Sera* 49
*6.3 Mpango wa Rasilimali wa Sera* 49
*6.4 Mkakati wa Mawasiliano* 50

## DIBAJI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliandaa Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2005 ambayo ilitoa muongozo wa kuimarisha maendeleo ya Vijana katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2005 imefanyiwa mapitio kutokana na matakwa ya kisera inayohitaji kufanyiwa mapitio kila baada ya miaka 5. Aidha, kutokana na mabadiliko ya sera za kiuchumi hasa muelekeo wa Serikali kiuchumi ambao umejikita zaidi katika kuimarisha uchumi wa buluu ambao unajumuisha mafuta na gesi, bandari, utalii na uvuvi wa ufugaji wa mazao ya bahari na kilimo cha mwani hususan kwa Vijana wa kike.

Pia, kutokana na mabadiliko ya kijamii yanayotokana na ukuaji wa sekta ya elimu na afya, ongezeko la idadi ya Vijana kwa mujibu wa sensa ya watu na makaazi kutoka asilimia 36.24 mwaka 2012 hadi asilimia 37.3 kwa mwaka 2022. Vile vile, ongezeko la muamko wa Vijana katika kushiriki na kushirikishwa katika maendeleo ya kisiasa na kuimarika kwa demokrasia Nchini.

Uanzishwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar ni sababu nyengine iliyopelekea kuwaunganisha na kuimarisha ushiriki wa Vijana katika shughuli za maendeleo na ujenzi wa Taifa. Hata hivyo, sera ya mwaka 2005 ilitaja uanzishwaji wa Baraza tu na kukosa kuonesha nafasi na majukumu yake katika utekelezaji wa sera.

Aidha, sera hii mpya inazingatia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2020 – 2025, mpango wa maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Dira ya maendeleo ya Zanzibar ya 2050, mpango kazi wa Maendeleo ya Vijana wa Dunia 2000 na kuendelea (WPAY2000 and Beyond), malengo ya maendeleo endelevu ya Dunia (SDGs) 2030, mkataba wa Afrika kuhusu maendeleo ya Vijana (African Youth Charter) ya mwaka 2006 na sera ya Vijana ya jumuiya ya Afrika mashariki 2013. Sera hii pia inalenga kuwajengea uwezo Vijana katika sekta ya uchumi wa buluu na kuwafikisha katika mpango wa Kitaifa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufikia uchumi wa kati.

Sera hii inatoa muongozo utakaoimarisha ustawi na maendeleo ya Vijana Nchini na kukabiliana na changamoto mbali mbali zikiwemo ukosefu wa ajira, athari za matumizi ya dawa za kulevya, upungufu wa kinga mwilini (UKIMWI), homa ya ini, fistula, Afya ya akili, ukosefu wa elimu wa Afya ya uzazi, ndoa za mapema, upatikanaji wa taarifa zinazohusu masuala ya Vijana, udhalilishaji wa kijinsia, Ushiriki na Ushirikishwaji mdogo wa Vijana katika ngazi mbali mbali za maamuzi na hatua za kujikwamua kiuchumi. Vile vile, sera hii inatoa muongozo kuhusu uimarishaji wa malezi, makuzi, maadili, uzalendo, amani, umoja, utulivu, demokrasia, elimu na afya. Aidha, sera imekusudia kuimarisha uratibu na usimamizi wa shughuli na programu za maendeleo na ustawi wa Vijana Nchini, pamoja na kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Baraza la Vijana Zanzibar, Asasi zisizo za kiserikali za Vijana na wadau wote wa maendeleo ya Vijana Nchini.

Napenda kutoa wito kwa wadau wote wa maendeleo ya Vijana Nchini kuipokea, kuzingatia na kuitekeleza sera hii kwa kuhakikisha wanaingiza masuala yanayohusu maendeleo ya Vijana katika sera, mipango na kuwashirikisha Vijana katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli mbali mbali za kimaendeleo ili kuimarisha mustakbali mwema na maendeleo ya Vijana wetu na Taifa kwa ujumla. Ni matumaini yangu kwamba mafanikio ya utekelezaji wa Sera hii yatapatikana kwa njia ya mashirikiano baina ya Vijana, taasisi za kiserikali , asasi za kiraia, washirika wa maendeleo, taasisi za kidini, jamii, wazazi na familia kwa ujumla.



**Tabia Maulid Mwita (MBM)**
**Waziri wa Habari, Vijana,**
**Utamaduni na Michezo**
**Zanzibar**

## SHUKURANI

Zoezi la kuifanyia mapitio sera ya maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005 na kuandaa sera mpya ya mwaka 2023 lilishirikisha wadau mbali mbali wa maendeleo ya Vijana Nchini wakiwemo watu binafsi, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali , washirika wa maendeleo, Baraza la Vijana, taasisi za kidini na Vijana wenyewe.

Wizara inapenda kutoa shukrani za dhati kwa shirika la umoja wa mataifa la idadi ya watu Duniani (UNFPA) kwa kubeba dhamana kubwa ya kusaidia hatua zote za mapitio ya Sera hii. Shukurani hizi ziwaendee pia Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), International Republican Institute (IRI) na United States Agency for International Development (USAID) kwa msaada wao uliosaidia kuwezesha kukamilisha sera hii.

Shukurani za kipekee kwa walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kukamilisha sera hii wakiwemo; taasisi za Serikali , asasi za kiraia, taasisi za kidini, Baraza la Vijana Zanzibar, waandishi wa habari na vyombo vyao vya habari pamoja na Vijana kwa ujumla.

Shukurani maalumu kwa uongozi mzima na watendaji wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na kamati ya wataalam ya wizara kwa juhudi zao katika kuhakikisha sera hii inakamilika. Aidha, napenda kuwashukuru wale wote waliochangia kwa njia moja au nyengine katika kukamilisha kazi hii.



**Fatma Hamad Rajab**
**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Habari, Vijana,**
**Utamaduni na Michezo**
**Zanzibar**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Vijana duniani kote wanatambulika kuwa ni rasilimali muhimu na yenye uwezo wa kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo ni lazima kutambulikana huko kuende sambamba na uwekezaji katika kuimarisha ustawi na maendeleo yao, huku tukiimarisha ushiriki wao katika shughuli za maendeleo ya Taifa. Karne hii mpya huwapatia Vijana fursa ya kushiriki na kushirikishwa katika shughuli za maendeleo kwa sababu wao ndio viongozi wa sasa na wa baadae. Kwa vile Vijana hawaishi peke yao wanatakiwa kujiandaa na kuandaliwa kuchukua nafasi ya kuongoza jamii

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya Vijana Nchini na Vijana wenyewe wanatakiwa kuandaa utaratibu, miongozo, programu na muelekeo wa maendeleo na ustawi wa Vijana Nchini. Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005 iliandaliwa na Serikali kwa ajili ya kuratibu na kusimamia ustawi na maendeleo ya Vijana Nchini. Hivyo sera ya maendeleo ya Vijana ya mwaka 2023 inalenga kuimarisha maendeleo na ustawi wa Vijana katika nyanja mbali mbali zikiwemo elimu, afya, elimu ya ufundi na mafunzo ya amali, ujasiriamali, kilimo, ajira, teknolojia ya habari na mawasiliano, ushiriki na ushrikishwaji, jinsia, stadi za maisha, afya ya uzazi, ubunifu, uongozi, uzalendo, uwajibikaji, utamaduni, sanaa, uchumi wa buluu pamoja na kushiriki katika michezo kwa lengo la kujenga afya na kupata ajira.

### 1.1 Usuli

Baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, Serikali iliwapatia Vijana fursa nyingi na muhimu kwa lengo la kuwaendeleza na kuwasaidia kimaisha ili kuliinua Taifa kiuchumi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye miaka ya 1960 na 1970 ilianzisha na kuziendeleza kambi maalumu kwa Vijana. Lengo la kambi hizo ni kuwapatia elimu ya uzalendo, ujasiri, ujuzi na kulinda amani ya

Nchi . Mbali na hatua hiyo, Serikali kwenye miaka hiyo iliwapeleka Vijana nje ya Nchi kwa lengo la kwenda kujifunza mipango na programu za kujiendeleza.

Kambi za Vijana ziliratibiwa na kusimamiwa na Umoja wa Vijana wa "Afro Shirazi Party" (ASPYL) na hatimae Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, Vijana walikuwa na viti maalum katika Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Shughuli za maendeleo ya Vijana kiserikali zilikuwa zinatekelezwa kiujumla wake kupitia sera, mipango na programu mbali mbali zilizokuwa zikitekelezwa na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kuimarisha shughuli hizo mwaka 1988 Serikali iliamua kuanzisha Idara ya Wanawake na Vijana iliyokuwa chini Wizara ya Nchi Ofisi ya Waziri kiongozi Zanzibar na hatimae Mwaka 1992 kuundwa rasmi Idara ya Maendeleo ya Vijana iliyokuwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Vijana Zanzibar kwa lengo la kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo na ustawi wa Vijana Nchini.

Pamoja na kuanzishwa kwa Idara ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar, Serikali iliona ipo haja pia ya kuweka muongozo rasmi wa namna ya kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Vijana Nchini. Sera ya maendeleo ya Vijana ilitayarishwa mwaka 2005 chini ya Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na watoto Zanzibar kwa ajili ya kuweka msingi imara wa utekelezaji, uratibu na usimamizi wa shughuli za maendeleo na ustawi wa Vijana Nchini. Miongoni mwa misingi iliyowekwa na sera hiyo ni kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana kwa uanzishwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar, elimu na mafunzo ya amali kwa Vijana, stadi za maisha, kuzijengea uwezo asasi za maendeleo ya Vijana, kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa Vijana, kuimarisha miundo mbinu ya michezo na burudani pamoja na kuimarisha afya zao ikiwemo kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI na matumizi ya dawa za kulevya

## 1.2 Upeo wa Sera

Maendeleo ya Vijana ni suala mtambuka, linalohitaji ushiriki wa sekta mbali mbali ili kufanikisha utekelezaji wake. Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ni miongoni mwa sera zilizotayarishwa na Serikali kwa ajili ya kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa Vijana yatakayowawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Sera hii itatekelezwa kwa kujumuisha na kushirikisha taasisi za Serikali kupitia sera, mipango na programu mbali mbali zitakazoimarisha ustawi na maendeleo ya Vijana Nchini. Aidha taasisi zisizo za kiserikali na wadau wote wa maendeleo ya Vijana Nchini, jamii na Vijana wenyewe watapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia matakwa ya sera hii.

## 1.3 Uhusiano na Sera nyingine za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

Sera hii ya maendeleo ya Vijana Zanzibar imezingatia na kuhusisha vipaumbele vya sera, mipango na mikataba mbali mbali ya Kimataifa , Kikanda na Kitaifa inayohusiana na ustawi na maendeleo ya Vijana. Miongoni mwa sera, mipango na mikataba hiyo ni kama ifuatayo: -

1.3.1 *Mpango wa Utekelezaji wa Maendeleo ya Vijana wa Dunia wa mwaka 2000 na kuendelea.*

Madhumuni ya mpango huu ni kuzihamasisha jumuiya za Kimataifa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo na ustawi wa Vijana katika uandaaji na utekelezaji wa sera, mipango, mikakati na programu za maendeleo ya Nchi . Vipaumbele hivyo ikiwemo; elimu, ajira, afya, usawa wa kijinsia, ushiriki na ushirikishwaji, uimarishaji wa amani na usalama, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), utunzaji wa mazingira, utandawazi, michezo na burudani, vita dhidi ya dawa za kulevya, virusi vya UKIMWI (VVU) na upungufu wa kinga mwilini (UKIMWI).

### 1.3.2 *Mkataba wa Vijana wa Afrika (2006)*

Mkataba wa Vijana wa Afrika umeweka misingi bora kwa mataifa ya Afrika juu ya kuimarisha ustawi na maendeleo ya Vijana pamoja na kuwalinda dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote. Mkataba umesisitiza pia haki mbali mbali za Vijana ikiwemo; haki ya kutembea, kulindwa, kujieleza, kujiunga pamoja, kuabudu, kumiliki mali, elimu, ajira, afya na ushiriki na ushirikishwaji. Aidha mkataba umeeleza wajibu wa Vijana katika utunzaji wa amani na usalama, mazingira, utamaduni, kuimarisha usawa wa kijinsia na kufuata utawala wa sheria.

### 1.3.3 *Sera ya Vijana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2013*

Sera ya Vijana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki nayo pia imetoa muongozo na kuweka mikakati madhubuti kwa Nchi wanachama kuwawezesha na kuwaendeleza Vijana katika masuala ya afya, elimu na mafunzo, TEHAMA, ajira na michezo. Aidha sera hii imezungumzia haki, uhuru na wajibu wa Vijana.

### 1.3.4 *Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050*

Dira ya maendeleo ya Zanzibar 2050 imeweka mkazo katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya Vijana ikiwa ni nguvu kazi Taifa na sehemu ya wananchi wa Zanzibar kupitia mabadiliko ya kiuchumi katika nyanja za kilimo, biashara, viwanda, utalii na uchumi wa buluu. Aidha dira imetoa msisitizo katika elimu na mafunzo kwa Vijana, afya, ajira, hifadhi ya jamii, utamaduni, michezo na teknolojia ya habari na mawasiliano.

### 1.3.5 *Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021 - 2026 (ZADEP)*

Mpango wa maendeleo wa Zanzibar umeweka mikakati madhubuti ya kujenga mazingira rafiki na wezeshi kwa maendeleo na ustawi wa Vijana. miongoni mwa mikakati hiyo ni kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kutoka asilimia 19.7 kwa mwaka 2020/2021 hadi asilimia 10 kwa mwaka 2025/2026, kuongeza idadi na nafasi za ushiriki katika vyombo vya maamuzi kwa Vijana,

Wanawake na watu wenye ulemavu kufikia asilimia 40 ifikapo mwaka 2025/ 2026.

Aidha mpango umedhamiria kuongeza idadi ya wanafunzi katika mafunzo ya amali hadi kufikia asilimia 70% ifikapo 2025/2026, kuongeza pia wanafunzi wa mafunzo ya kidigitali kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025/2026 na kupunguza vitendo vya udhalilishaji wa Wanawake na watoto kwa asilimia 85 ifikapo 2025/2026.

### 1.3.6 *Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025*

Ilani ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2020-2025 inaenda sambamba na Sera ya Maendeleo ya Vijana ambapo katika Ibara ya 210 imeweka mkazo kuwawezesha Vijana kimaendeleo katika nyanja mbali mbali ikiwemo upatikanaji wa ajira 300,000, kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya amali hadi kufikia 47,000, kuwapatia Vijana 5000 mafunzo ya uongozi, kuwapatia Vijana 100,000 elimu ya malezi, uzalendo, moyo wa kujitolea na kuipenda Nchi yao pamoja na kuimarisha utoaji wa mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

### 1.3.7 *Sera ya Sekta ya Kilimo Zanzibar (2002)*

Sekta ya kilimo inajumuisha mazao, uvuvi, na ufugaji. Lengo kuu la Sera ya Kilimo ni kukuza maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo ili iweze kutoa faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira. Sera hii inawiana na Sera ya Maendeleo ya Vijana kwa kuimarisha miundombinu bora na ya kisasa itakavyowavutia Vijana kuingia katika sekta ya kilimo pamoja na kuongeza uzalishaji ili kujitosheleza kwa chakula na kutoa mchango sawia katika kukuza uchumi wa Taifa na kuimarisha fursa za ajira kwa Vijana.

### 1.3.8 *Sera ya Uwekezaji Zanzibar (2005)*

Sera hii imeweka malengo ya ujumla ambayo yameelekezwa katika sekta za vipaumbele ambazo ni pamoja na huduma za biashara na fedha, bandari huru na kukuza sekta ya utalii kama msingi wa maendeleo ya kiuchumi Nchini.

Uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kusafirishwa na kuuzwa ndani na nje ya Nchi ,na kuendeleza sekta ndogo ndogo za uvuvi, bahari, biashara ya bidhaa na huduma. Sekta zote hizi za kipaumbele kwenye sera ya uwekezaji zinaweza kuendelezwa na Vijana waliowezeshwa katika mafunzo, mitaji na upatikanaji wa masoko.

### 1.3.9 *Sera ya Biashara Zanzibar (2006)*

Sera ya Biashara imetayarishwa na kupendekeza utekelezwaji wa taratibu wa kuzijengea uwezo biashara, ikiwa na msisitizo kwenye kuondoa vikwazo vya usambazaji na upatikanaji wa bidhaa mbali mbali kwa ubora wa bidhaa kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi . Pia, sera ina lengo la kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara Nchini pamoja na kuzingatia masuala ya kufanya biashara na mataifa ya nje. Udhibiti wa viwango na upatikanaji wa masoko ni muhimu sana kuzigatiwa katika Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar kwa lengo la kuimarisha bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara Vijana kwa kuwapatia mafunzo, masoko na mitaji ya kuendeleza biashara zao.

### 1.3.10 *Sera ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SMEs) Zanzibar (2006)*

Lengo la jumla la sera hii ni kujenga mazingira bora ya kuendeleza biashara ndogo na kati kwa lengo la kuongeza fursa za ajira na mapato. Aidha, sera hii imeweka mikakati ya kukuza sekta ya wajasiriamali wadogo na wa kati, kuendeleza biashara ndogo ndogo kwa kuimarisha ujuzi, masoko, upatikanaji wa mitaji, kuongeza thamani ya mazao pamoja na kuweka misingi bora ya kodi. Utekelezaji wa Sera hii utaimarisha hali za kiuchumi kwa Vijana na kuongeza fursa za ajira Nchini.

### 1.3.11 *Sera ya Elimu Zanzibar (2006)*

Madhumuni ya Sera ya Elimu ni kuandaa mfumo imara wa elimu wenye uwezo wa kutoa majibu kwa changamoto za kielimu ambao Vijana ndio wanufaika wakuu. Sera hii inalenga kutoa fursa, usawa, elimu bora kwa wote na kukuza taaluma endelevu kwa Vijana, ili kuhakikisha Vijana wanakuwa wanaelimika

na kuleta mabadiliko chanya katika maendeleo ya Zanzibar pamoja na kutumia elimu yao katika kukabiliana na changamoto za kimaisha zinazowakabili.

### 1.3.12 *Sera ya Ajira ya Zanzibar (2009)*

Sera ya Ajira imedhamiria kutengeneza fursa kwa Vijana kupata ujuzi utakaoendana na soko la ajira ili Vijana kujiajiri na kuajiriwa. Aidha sera hii imesisitiza upatikanaji wa fursa sawa za ajira kwa Vijana wa kike na wa kiume pamoja na Vijana wenye ulemavu. Sera hii pia imekusudia kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa sekta isiyo rasmi ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kuzalisha ajira zaidi na zenye staha kwa Vijana.

### 1.3.13 *Sera ya Mifugo Zanzibar (2011)*

Madhumuni ya Sera ya Mifugo Zanzibar ni kujenga sekta ya mifugo yenye kustawi itakayochangia kipato kwa familia, kuwa na uhakika wa chakula, kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa na kupunguza umaskini. Aidha Sera hii ina lengo la kujenga mazingira rafiki na kisasa ili kuimarisha uwekezaji na kuzalisha ajira zaidi katika sekta binafsi kupitia ukuzaji wa masoko ya bidhaa za asili na zisizo za asili utakaozingatia uhifadhi na utunzaji wa mazingira na maliasili za Taifa kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

### 1.3.14 *Sera ya Afya Zanzibar (2011)*

Vijana ni nguvu kazi ya Taifa, ili nguvu kazi hiyo iweze kutumika vizuri na kuleta tija kwa Taifa, afya bora ndio jambo la msingi. Sera ya Maendeleo ya Vijana inaenda sambamba na Sera ya Afya Zanzibar ambayo ina lengo la kuhakikisha Wananchi wote wa Zanzibar wanakuwa na afya njema pamoja kuwapatia huduma bora za kinga na tiba. Aidha, kuimarisha upatikanaji wa haki ya huduma bora za afya kwa misingi ya usawa na kwa kuzingatia viwango na ubora vilivyowekwa kupitia afya ya msingi (Primary Health Care). Sera pia imeekeza nguvu katika kuimarisha miundombinu na programu za elimu ya

afya ikiwemo afya za uzazi na mtoto, kifua kikuuu, ukoma, homa ya ini, malaria, pamoja na maradhi mengine ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

### 1.3.15 *Sera ya Utawala Bora Zanzibar (2011)*

Madhumuni ya Sera ya Utawala Bora ni kujenga mazingira wezeshi na endelevu kwa ajili ya uimarishaji wa utawala bora kwa kuheshimu haki za binaadamu na utawala wa sheria, kuzuia rushwa na kuhakikisha kwamba misingi ya uwajibikaji, uwazi, ufanisi na tija, ushirikishwaji na kuzingatia matakwa ya Wananch yanaheshimiwa. Sera hii inahusiana na Sera ya Maendeleo ya Vijana kwa kuwahimiza Vijana kuishi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora ikiwemo kuheshimu haki za binaadamu na utawala wa sheria, kujiepusha na vitendo vya rushwa, kuwa wawajibikaji katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo kwa maslahi yao na Taifa kwa ujumla. Aidha, sera inawahimiza Vijana kuwa wawazi, kuongeza ufanisi na tija, kuwa tayari kushiriki na kushirikishwa ili kujenga uelewa juu ya dhana ya utawala bora.

### 1.3.16 *Sera ya Taifa ya Ukimwi Zanzibar (2012)*

Lengo kuu la sera hii ni kutoa muongozo sahihi na kuchukua hatua stahiki za kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI hususan kwa Vijana wa kike na wakiume, kutoa tiba na kuwaunga mkono watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ili kuweza kupunguza athari za maambukizi ya ukimwi kwa kuchukua jitihada za makusudi kwa kushirikiana na wadau mbali mbali. Sera hii inalenga kutumia mbinu ya kushirikisha sekta mbali mbali kwa ajili ya kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa makundi yaliyopo katika mazingira hatarishi wakiwemo Wanawake, vijana na makundi yenye mahitaji maalumu.

### 1.3.17 *Sera ya Mazingira Zanzibar (2013)*

Madhumuni ya kuanzishwa kwa Sera ya Mazingira Zanzibar ni kwa lengo la kuonesha njia bora ya kulinda, kuhifadhi, kuboresha na kudhibiti rasilimali za mazingira zilizopo Zanzibar. Sera hii imejikita katika kutoa miongozo ikiwemo

upatikanaji au utunzaji wa mazingira kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ambayo itapunguza uzalishaji na uondoshaji wa taka pamoja na kuwashirikisha Vijana katika utunzaji, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira ikiwemo kuzibadilisha taka hizo kuwa malighafi ya uzalishaji wa bidhaa na kupelekea kuongezeka kwa ajira kwa Vijana.

#### 1.3.18 *Sera ya Ushirika Zanzibar (2014)*

Madhumuni makubwa ya sera hii ni kukuza uchumi wa Taifa kwa kutoa mkazo katika umiliki wa uchumi kwa watu na kupunguza umasikini wa kipato, kutengeneza fursa zaidi za ajira katika sekta binafsi pamoja na kuimarisha huduma za kifedha kwa wanaushirika kupitia vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa (SACCOS). Sera hii pia inaimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika shughuli za kiuchumi kupitia kuanzisha na kujiunga na vyama vya ushirika, upatikanaji wa mafunzo na mikopo ya miradi wanayoianzisha.

#### 1.3.19 *Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar (2014)*

Sera inajumuisha mifumo ya hifadhi wa jamii na misaada kwa jamii. Hifadhi ya jamii ni muhimu sana kwa ajili ya kupunguza na kuondoa umaskini na kuleta usawa katika jamii. Hivyo sera hii ina mahusiano moja kwa moja na Sera ya Maendeleo ya Vijana kwa kusaidia wajasiriamali Vijana kwa kuendeleza na kuwaekea hifadhi kile wanachokipata kutokana na biashara zao ili kiwasidie kwa maisha yao ya sasa na baadae.

#### 1.3.20 *Sera ya Jinsia Zanzibar (2016)*

Sera ya Jinsia ya 2016 ina lengo la kuimarisha usawa wa kijinsia na kukuza ushiriki na uwezeshaji Wanawake ikiwemo Vijana wa kike katika masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, pamoja na kukuza ushiriki katika ngazi za uongozi na kufanya maamuzi, uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika sera na sheria, mipango, programu na bajeti katika ngazi zote. Aidha, Sera hii

inahimiza uzingatiaji wa mahitaji ya kijinsia na umiliki pamoja na ugawaji wa rasilimali na kuendelea kupiga vita vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia vinavyowakabili zaidi Vijana wa kike na watoto.

### 1.3.21 *Sera ya Uvuvi Zanzibar (2016)*

Sera hii imelenga kukuza uzalishaji katika sekta ya uvuvi kwa kuongeza kiwango cha upatikanaji wa bidhaa za uvuvi, kuongeza thamani na ubora wa samaki sambamba na usalama kulingana na mahitaji ya watumiaji ndani ya jamii ya Zanzibar ili kuweza kufikia viwango vya biashara katika soko la Kimataifa . Pia, sera hii itaimarisha uvuvi wa kisasa ambao utaleta kipato na kuzalisha ajira zaidi kwa Vijana kwa kutumia teknolojia na mbinu za kisasa.

### 1.3.22 *Sera ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar (2018)*

Sera hii inaimarisha ustawi na maendeleo ya watu wenye ulemavu wakiwemo Vijana kwa kuzingatia haki na fursa za watu wenye ulemavu kwa mujibu wa uwezo waliokuwa nao, pamoja na kutengeneza mazingira rafiki yatakayowawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Mkazo zaidi umeweka kuimarisha uwezo, ulinzi na huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu pamoja na kuzingatia mahitaji yao.

### 1.3.23 *Sera ya Utalii Zanzibar (2018)*

Sera ya Utalii inasisitiza ushiriki wa wadau wa utalii wakiwemo Vijana kuwa wabunifu na wawe tayari kupokea na kutumia teknolojia za kisasa na zilizorahisishwa katika kufanya kazi zao ili kukidhi matarajio ya wateja katika njia mbali mbali. Sera ya Utalii ina mahusiano makubwa na Sera ya Maendeleo ya Vijana, kwa kuzingatia kuwa Vijana ni wazalishaji wakubwa wa bidhaa na watowaji wa huduma katika sekta ya utalii.

1.3.24 *Sera ya Michezo Zanzibar (2018)*

Sera ya Michezo Zanzibar imeweka utaratibu wa Kitaifa wa kuwawezesha watu wote ikiwemo Vijana kushiriki katika michezo kwa maendeleo ya kijamii, kielimu, kiuchumi na kiafya pamoja na kuibuwa, kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo kwa Vijana, kuimarisha miundombinu na kutoa mafunzo ili waweze kushiriki na kushindana katika michezo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa .

1.3.25 *Sera ya Diaspora Zanzibar (2018)*

Uwepo wa Sera ya Diaspora Zanzibar unasaidia kutafuta na kuelekeza matumizi sahihi ya fursa mbali mbali zitakazosaidia katika kuharakisha maendeleo ya Zanzibar. Fursa hizo ni pamoja na misaada ya kifedha, uwekezaji, taaluma, ujuzi na teknolojia. Hivyo Sera hii inatoa muongozo kuhusu namna wanadiospora wa Zanzibar ambao wengi wao ni Vijana kushiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo ya Nchi yao ya asili.

1.3.26 *Sera ya Taifa ya Ardhi Zanzibar 2018*

Sera ya Ardhi inasimamia haki ya upatikanaji wa ardhi, matumizi bora na usimamizi wake kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kuchumi kwa Wananch wa Zanzibar. Ardhi inatakiwa ionekane kama ni mtaji wa kuongeza uzalishaji na mafanikio ya kiuchumi. Vijana ni nguvu kazi ya Taifa hivyo sera inatowa fursa kwa Vijana kuweza kuitumia ardhi katika shughuli mbali mbali za kiuchumi na kijamii ili kuimarisha ustawi na maendeleo yao na Taifa

1.3.27 *Sera ya Viwanda Zanzibar (2019)*

Sera ya Viwanda imedhamiria kujenga na kuimarisha jitihada za Kitaifa za kuimarisha maendeleo ya biashara ndogo na za kati na kuweka mfumo wa ukuzaji uchumi unaoongozwa na sekta binafsi.

Sera hii pia itaimarisha sekta ya viwanda vidogo vidogo na vya kati ili kuimarisha mpango wa kuongeza ajira na kupunguza umasikini Nchini. Vile

vile mikakati ya wazi imewekwa ya kuwajengea uwezo wa kitaaluma na nyenzo Vijana ili waweze kuwa wabunifu na kuongeza thamani ya mazao au bidhaa zinazozalishwa Nchini kupitia uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo na vya kati vitakavyozalisha ajira zaidi kwa Vijana na kuinua uchumi wa Nchi .

1.3.28 *Sera ya Uchumi wa Buluu Zanzibar (2020)*

Sera hii imeweka mikakati ya kuimarisha uwekezaji katika sekta ya utalii, mafuta na gesi, uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha mwani, ufugaji wa samaki na majongoo, uvunaji wa chumvi, viwanda vidogo vidogo vya kusindika bidhaa na kukuza ubora wa bidhaa na masoko.

Uwekezaji huo utaimarisha na kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii pamoja na kuongeza fursa za ajira kwa Vijana zitakazowapelekea kujiajiri na kuajiriwa katika sekta rasmi na isiyo rasmi.

1.3.29 *Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali Zanzibar (2020)*

Sera hii inadhamiria kuimarisha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali kwa Vijana kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo katika jamii na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Uimarishaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali utasaidia Vijana kupata ujuzi na taaluma itakayowapelekea kuwa na sifa pamoja na vigezo vitakavyowapelekea kuingia na kukabiliana na ushindani wa soko la ajira na kukuza ajira binafsi kwa Vijana ili kujikwamua na umasikini.

1.3.30 *Sera ya Uwezeshaji Wananch Kiuchumi Zanzibar (2022)*

Sera ya Uwezeshaji Wananch Kiuchumi Zanzibar ina lengo la kuimarisha uratibu na usimamizi wa shughuli za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi Zanzibar. Aidha, kukabiliana na changamoto za kiuwezeshaji zinazowakabili vijana, Wanawake na makundi yenye mahitaji maalum. Msisitizo zaidi umewekwa katika utoaji wa mafunzo, mitaji na masoko kwa biadhaa zinazozalishwa na wajasiriamali Nchini.

1.3.31 *Rasimu ya Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (2023)*

Sera hii imesisitiza kuwa na jamii iliyoepukana na dawa za kulevya ili kuhifadhi nguvu kazi ya Taifa kwa maendeleo ya Zanzibar, kwa kuongeza nguvu zaidi katika udhibiti usafirishaji, usambazaji, utengenezaji, matumizi na kupunguza athari za dawa za kulevya kiafya, kijamii na kiuchumi kwa kuanzisha na kuimarisha utekelezaji wa mifumo ya kisheria, kitaasisi, programu, uhamasishaji jamii na mashirikiano yanayolenga mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Sera hii inasaidia moja kwa moja utekelezaji wa sera ya maendeleo ya Vijana kuimarisha malezi, makuzi na maadili bora kwa Vijana ili kuwa na Vijana ambao ni raia wema na wenye tija kwa Nchi yao.

## SURA YA PILI

### 2.0 HALI HALISI YA VIJANA ZANZIBAR

Tafsiri ya kijana inatofautiana baina ya Nchi moja na nyengine. Umoja wa Mataifa unatafsiri kuwa kijana ni kuanzia umri wa miaka 15 hadi 24 wakati Umoja wa Afrika unatafsiri kijana ni kati ya umri wa miaka 15 hadi 35. Sera hii inakwenda sambamba na tafsiri ya Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2005 ambayo pia inaenda sambamba na tafsiri ya kijana ya Umoja wa Afrika inayoelezea kuwa kijana ni mtu mwenye umri kuanzia miaka 15 hadi 35. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Zanzibar ina jumla ya wakaazi wapatao 1,889,773 ambapo Vijana ni 699,845 sawa na asilimia 37.3 (Wanawake ni 368,066 na Wanaume ni 331,779).

### 2.1 Vijana na Afya

Vijana ni miongoni mwa makundi yanayoathirika na maradhi mbali mbali ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Vijana wengi hupata maambukizi ya maradhi ikiwemo; UKIMWI, afya ya akili, tatizo la afya ya uzazi, kifua kikuu, festula na maradhi mengine ya kujamiiana kama vile kaswende na kisonono kutokana na uelewa mdogo wa elimu ya afya. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti (THS 2016) uliofanywa na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Zanzibar imeripotiwa kupungua kwa maambukizo ya VVU kutoka asilimia 1% hadi 0.4% Takwimu zinaonesha pia jumla ya watu 7,598 (Wanaume 40.4% na 59.6% Wanawake) wanaishi na Virusi vya UKIMWI.

Tatizo la afya ya uzazi kwa Vijana linajumuisha ukosefu wa taaluma na taarifa sahihi juu ya afya ya Uzazi, haki na uhuru wa kuzaaa na kupanga watoto pamoja na haki ya upatikanaji ya huduma za afya ya uzazi kwa kuzingatia mahitaji na wakati unaofaa. Pia tatizo la afya ya uzazi kwa Vijana linahusisha ndoa za mapema na mimba zisizotarajiwa.

Vijana wengi wanakabiliwa na changamoto nyingi za afya ya uzazi zinazopelekea kuwa katika hatari ya kupata matatizo ya afya ya akili, fistula,

msongo wa mawazo, mimba zisizotarajiwa, kutengwa na familia, umasikini na kujiingiza katika vitendo vya uasharati.

### 2.2 Vijana na Uzalendo

Mambo muhimu ya kuzingatia ili kuwa raia mwema na mzalendo ni pamoja na kuipenda, kuiheshimu na kuithamini Nchi yako, kuwa muwajibikaji, kuwa mstahamilivu, kuwa mwadilifu, mwenye kutii na kufuata utawala wa sheria pamoja na kudumisha amani, utulivu na umoja Nchini.

Vijana wa Zanzibar kama vile Vijana wengine Duniani wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la ukosefu wa uzalendo. Hata hivyo bado kumekuwa na taasisi na program za kizalendo, miongoni mwa shughuli hizo ni makambi ya kujitolea, ujenzi wa Taifa, utoaji wa Huduma ya kwanza na kusaidia wakati wa majanga.

Uzalendo ni changamoto kwa Vijana wa Zanzibar hasa kwa miaka hii ya karibuni. Hali hii inatokana na ukosefu wa elimu sahihi ya historia ya Nchi , elimu ya uraia, mgawanyiko wa jamii, tofauti ya mitazamo, siasa, uelewa mdogo wa dini na mmongo'nyoko wa maadili. Kukosekana kwa uzalendo Nchi hupelekea kupoteza thamani, rasilimali, maendeleo na amani. Hali hii husababisha Vijana kujiingiza katika biashara haramu, vikundi viovu vya itikadi kali na hatimae ugaidi.

### 2.3 Vijana na Utawala Bora

Chimbuko la utawala bora Zanzibar linatokana na sheria na katiba ya Zanzibar, ambapo pamoja na mambo mengine imeweka bayana utawala wa sheria na misingi ya usawa na haki za binaadamu. Vijana wenye umri kati ya miaka 18 – 35 ndio kundi kubwa linaloshiriki katika uimarishaji na uendelezaji wa demokrasia, utawala bora pamoja na amani na utulivu Nchini. Miongoni mwa shughuli wanazoshiriki na kushirikishwa Vijana Zanzibar ni kushiriki katika shughuli za siasa ndani ya vyama vya siasa, kuchagua na kuchaguliwa katika chaguzi za ngazi mbali mbali za maamuzi, kupiga vita rushwa na kujitolea katika matukio mbali mbali ya kijamii.

Pamoja na ushiriki huo bado Vijana wanakabiliwa na changamoto kama vile ukosefu wa elimu sahihi ya utawala bora na demokrasia, mwamko mdogo wa Vijana kujua haki zao za msingi ikiwemo kupata hati za utambulisho, fursa za ajira, kushiriki katika shughuli za kimaendeleo na utii wa sheria za Nchi mambo ambayo yakikosekana hupelekea vitendo viovu, uvunjifu wa amani na kuzorotesha maendeleo ya Nchi

### 2.4 Vijana na Stadi za Maisha

Programu za stadi za maisha ni mpango kabambe wa malezi na makuzi ya Vijana, unaotilia mkazo suala la kujitambua, kuweka malengo na jinsi ya kufanikisha malengo yao ya maisha. Elimu hiyo ya stadi za maisha kwa Vijana inajumuisha vitu kama vile stadi za mawasiliano, utoaji wa maamuzi, uwezo wa kuhimili mihemko, ushawishi na utetezi, kukabiliana na shindikizo rika. Pamoja na uwepo wa muongo wa stadi za maisha bado kuna changamoto zinazowakabili Vijana katika upatikanaji wa elimu ya stadi za maisha zikiwemo kutokuwepo kwa programu madhubuti zinazowashirikisha wadau mbalimbali katika utowaji wa elimu za stadi za maisha, ushiriki mdogo wa wazazi katika kuwapatia Vijana stadi za maisha na mporomoko wa maadili na tabia za Vijana kutokana na kukosekana kwa stadi za maisha.

### 2.5 Vijana na Ajira

Ukosefu wa ajira ni moja kati ya changamoto inayowakabili Vijana wengi Zanzibar na ulimwengu kwa ujumla.  Utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi Tanzania (ILFS) 2020/2021, inaonesha kwamba Zanzibar ina kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kwa Vijana wenye umri wa miaka 15 - 35 ambao ni sawa na asilimia 27.6 ukilinganisha na asilimia 12.2 ya Vijana kwa upande wa Tanzania Bara. Utafiti huo unaonesha pia ukosefu wa ajira kwa Vijana wa kike ni mkubwa zaidi ambao sawa na asilimia 40.7 ukilinganisha na Vijana wa kiume ambao ni asilimia 15.5 wenye umri kati 15 – 35 (*Utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi 2020/2021*).

Katika kukabiliana na tatizo hilo Serikali imeanzisha programu mbali mbali za kuwezesha ajira kwa Vijana, zikiwemo kuanzisha wakala wa uwezeshaji Wananchi kiuchumi (ZEEA), kuanzisha amlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Bandari huru, programu za ajira kwa Vijana, kuanzisha vituo cha kukuza na kulea wajasiriamali, kuandaa mpango kazi wa ajira kwa Vijana (Zanzibar youth empolyment action plan), Baraza la Vijana la Zanzibar, kutenga asilimia nne ya mapato ya kila Halmashauri ya Zanzibar za kuwawezesha Vijana pamoja kuanzisha na kuendeleza vyuo vya mafunzo ya amali katika ngazi ya Wilaya na Mikoa yote ya Zanzibar. Aidha, katika kipindi cha Machi 2022 hadi Mei 2023, Serikali kupitia wakala wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi imetoa zaidi ya bilioni 18,189,933,292.40 kwa wajasiriamali 18,561 hususa Vijana ili waweze kujiinua kiuchumi na kujiajiri.

### 2.6 Vijana na Elimu

Serikali imekuwa ikitilia mkazo zaidi suala la elimu kwa Vijana kwa kuimarisha upatikanaji wa elimu. Vijana wengi hupata fursa ya elimu ikilinganishwa na zamani. Idadi ya wanafunzi waliojiunga na skuli za umma na binafsi hadi kufikia mwaka 2022 kwa upande wa sekondari ni 103,289 ambapo kwa skuli za umma ni 90,606 na skuli za binafsi 12,683. Utafiti huo huo unaonesha kwamba idadi ya wanafunzi wanaojiunga na taasisi za elimu ya juu za Serikali imeongezeka kutoka 5,066 mwaka 2018 hadi 12,663 mwaka 2022 (Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii 2022). Serikali pia imeandaa mpango wa kuwarejesha Vijana waliotoroka na wasichana waliopata mimba za mapema wakiwa skuli. Hata hivyo, changamoto kubwa kwa sekta hii ni jinsi gani mfumo wa elimu hapa Zanzibar ulivyojikita katika kuwaandaa Vijana kuweza kukabiliana na changamoto za maisha. Kwa hivyo jitihada kubwa inahitajika kuuwezesha mfumo wa elimu kumuwezesha kijana kujiajiri na kuajirika kwa mujibu wa mahitaji ya soko la ajira

## 2.7 Vijana na Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Amali na Ujasiriamali

Serikali imetoa kipaumbele kwa mafunzo haya kwa kuchukua juhudi mbali mbali za kuimarisha sekta hizo zikiwemo kukipandisha hadhi Chuo cha Ufundi Karume na kuwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na kuanzisha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inayoratibu shughuli hizo pamoja na kujenga mazingira bora yaliyopelekea ongezeko la Vyuo vya Mafunzo ya Amali arubaini na saba (47) ambapo vya umma ni vituo kumi na nne (14) vinavyomilikiwa na taasisi mbali mbali za Serikali ikiwemo vitano (5) vilivyo chini ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali vilivyopo Mwanakwerekwe, Mkokotoni na Makunduchi kwa Unguja na Vitongoji na Daya kwa Pemba. Aidha, viko vituo thalasini na tatu (33) vilivyoanzishwa na kumilikiwa na taasisi na watu binafsi kwa lengo la kuwasaidia Vijana kupata mafunzo yatakayowasaidia kujiajiri na kuajiriwa.

Kwa upande wa ujasiriamali hakuna utafiti rasmi uliofanyika kufahamu idadi ya Vijana wanaojishughulisha na ujasiriamali lakini hali inaonesha kuwa Vijana huanzisha miradi ya kiuchumi isiyo rasmi kama mbadala wa ajira. Shughuli maarufu zinazofanywa na Vijana ni kilimo, uvuvi, ufugaji, useremala, biashara na nyengenezo. Pamoja na jitihada za Vijana kujiinua kiuchumi katika sekta isiyo rasmi lakini bado wanakabiliwa na ukosefu wa mazingira wezeshi na rafiki ya kufanyia kazi ikiwemo taaluma sahihi ya biashara, masoko, mifumo ya urasimishaji wa biashara pamoja na mitaji ya kuanzisha na kuendeleza shughuli zao. Aidha Vijana wa Zanzibar wanakabiliwa na mtazamo hasi juu ya suala la kujiajiri, kujituma na uwajibikaji kazini.

## 2.8 Vijana na Teknolojia na Ubunifu

Teknolojia hurahisisha matumizi ya mashine katika nyanja mbali mbali za kiuchumi kama vile, viwanda, kilimo, usafiri na usafirishaji pamoja na mawasiliano. Kadri ya siku zinavyokwenda mbele ndivyo dhana hii ya teknolojia inavyokua kwa kasi duniani na kuwashawishi watu wengi hasa Vijana kwenda sambamba na mabadiliko hayo yanayotokea.

Faida nyingi za teknolojia zimepatikana kwa Vijana. Miongoni mwao ni kuongezeka kwa ubunifu na ugunduzi, uzalishaji, mawasiliano ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, kuokoa muda, kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali watu, upatikanaji wa taarifa na kuifanya dunia kuwa kijiji kutokana na mitandao mbali mbali ya kijamii.

Licha ya faida hizo, zipo hasara zinazowakumba Vijana ambazo miongoni mwao ni kuathirika kiafya na kiutamaduni, kushirikishwa katika biashara haramu, vitendo vya kigaidi, kupoteza muda katika mitandao ya kijamii, kutuma na kusambaza picha na matukio yasiyofaa, kukashifu watu kwa kusambaza taarifa zisizokuwa sahihi, pamoja na ukosefu wa Elimu, uhamasishwaji na uendelezwaji wa vipaji vya Vijana wabunifu

### 2.9 Vijana Wenye Ulemavu na Wenye Mahitaji Maalumu

Jamii ya Wazanzibari imekuwa na muamko mzuri wa kuwajali, kuwathamini, kuwashirikisha na kuwaendeleza Vijana wenye ulemavu na Vijana wenye mahitaji maalumu katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Serikali inajitahidi vya kutosha katika kuwashirikisha Vijana wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum katika shughuli za kimaendeleo katika ngazi zote za kiserikali , kijamii, kisiasa na kiuchumi. Aidha Serikali imeridhia mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu (UNCRPD) wa mwaka 2009. Katika kushiriki na kuwashirikisha Vijana wenye ulemavu jitihada zinahitajika kuendelezwa katika kuelimisha jamii kuhusiana na Vijana wenye ulemavu na Vijana wenye mahitaji maalum katika kushirikiana nao kwenye nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii ili kulileteа maendeleo Taifa.

### 2.10 Vijana na Mazingira

Mazingira ni binadamu na mambo yote yanayomzunguka katika maisha yake, ikiwemo maumbile asilia, mandhari, ardhi, bahari, uoto wa mimea na wanyama ambao wamo katika maeneo yanayowazunguka. Mazingira huweza kuimarishwa na kutunzwa kutokana na uasili wa maeneo yalipo kabla na

baada. Vile vile, shughuli za kibinadamu zinaweza kuchangia uharibifu wa mazingira katika maeneo yanayoizunguka.

Serikali imekuwa ikijitahidi vya kutosha katika kutunza, kuhifadhi na kuendeleza mazingira ikiwemo kuridhia mikataba ya kikanda na Kimataifa ya kutunza na kuendeleza mazingira, kutengeza sera, sheria, kanuni na miongozo ya uhifadhi wa mazingira. Licha ya jitihada zote bado inaonekana Vijana wana uelewa mdogo juu ya kuhifadhi mazingira. mfano uchimbaji wa mchanga, ukataji wa miti, uharibifu wa matumbawe pamoja na utupaji ovyo wa takataka, mambo ambayo hupelekea mmong'onyoko wa ardhi na mabadiliko ya tabia Nchi .

### 2.11 Ushiriki na Ushirikishwaji wa Vijana

Ushiriki unaweza kuwa wa moja kwa moja au kwa njia ya kuwakilishwa. Ushiriki wa Vijana Zanzibar katika vyombo vya kutoa maamuzi ni mdogo sana. Katika Baraza la Wawakilishi, sera na sheria nyingi zinazohusu maendeleo ya Vijana zinajadiliwa na kupitishwa ambapo uwakilishi wa Vijana ni wa kiwango cha chini sana unaotokana na nafasi za vyama vya siasa.

Serikali katika kuhakikisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika ujenzi wa maendeleo ya Taifa lao, imeanzisha Baraza la Vijana kupitia Sheria nambari 16 ya mwaka 2013 linalotumika kama jukwaa la kuwaunganisha Vijana wote bila ya kuzingatia itikadi za kisiasa, dini au kabila kwa kutetea maslahi ya Vijana Nchini. Aidha mpango maalum wa kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa mwaka 2020 - 2025 umeandaliwa.

Taasisi nyingi zinazoanzishwa hapa Zanzibar hazizingatii ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana wa kutoa michango yao kwa maendeleo ya Nchi . Sera na sheria nyingi zilizopo hazijaweka wazi muelekeo na nafasi za Vijana kushiriki na kushirikishwa katika ngazi za maamuzi pamoja na umuhimu wao katika maendeleo ya Nchi .

## 2.12 Vijana na Usawa wa Kijinsia, Vita dhidi ya Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia

Harakati za ustawi na maendeleo ya Vijana Nchini zinapaswa kwenda sambamba na uimarishaji wa usawa wa kijnsia kwa Vijana wote wa kike na wakiume bila ya kujali jinsia, kabila, dini au hali zao za kijamii na kiuchumi. Serikali imefanikiwa kuimarisha ushiriki na uwezeshaji wa Vijana wa kike na kiume kupitia taasisi na majukuwaa yao ya Baraza la Vijana.

Pamoja na juhudi hizo bado matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya Vijana yamekuwa ni changamoto Zanzibar hususan kwa Vijana wa kike na watoto. Miongoni mwa matukio maarufu ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ni pamoja na ubakaji, ndoa za kulazimishwa, unyanyasaji wa kingono, vipigo, kutelekeza familia na mimba katika umri mdogo.

Kwa mujibu wa Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (2022) takwimu zimeonyesha kuwa matukio ya uzalilishaji ni 1,222 wakiwemo Wanawake 154 sawa na asilimia 12.6 na watoto 1,068 sawa na asilimia 87.4. Aidha kwa upande wa watoto wakike ni 846 sawa na asilimia 79.2 na watoto wa kiume 222 sawa na asilimia 20.8.

Hali hii inaonyesha kuwa matendo ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa Wanawake na Vijana Zanzibar yapo yanaongezeka kwa kasi kubwa kila mwaka na yanachangiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na ufahamu mdogo kati ya Wanawake na Vijana wenyewe katika jamii kwa ujumla. Hivyo, kuna haja ya kuwekwa mikakati ya kuondosha athari hizi kwa kuwekwa kwa sheria na adhabu kali kwa wahusika ili matendo haya yatokomezwe kabisa.

## 2.13 Vijana na Silka, Utamaduni na Sanaa

Utamaduni unaweza kuelezwa kuwa ni yale mambo yote yanayotendeka katika maisha ya kila siku ya watu katika mazingira yao zikiwemo mila, silka, desturi, itikadi, lugha, sanaa, na nyaraka na kumbukumbu za kihistoria, Sanaa ni matokeo ya juhudi za mwanadamu katika kupambana na mazingira yake. Sekta ya utamaduni na sanaa imekuwa ikiwapatia Vijana fursa mbalimbali

zikiwemo kupata ajira, kutambulikana na jamii, kuwa utambulisho wa Taifa pamoja na kutunza na kuimarika kwa utamaduni. Hata hivyo Vijana hawana uelewa wa kutosha kuhusu utamaduni wao, ambapo changamoto kubwa ni kutokana na utandawazi, Vijana kuchanganya tamaduni zao na tamaduni za nje ambazo nyengine haziendani na tamaduni zetu, hivyo hupelekea mmong'onyoko wa maadili ya Vijana kwa kuiga tamaduni hizo.

Vijana wamekuwa wakijishughulisha sana na shughuli za sanaa pamoja na kuwepo wasanii wenye uwezo, vipaji na ubunifu wa kuzalisha kazi za sanaa mbali mbali. Hata hivyo kumekuwa na vikwazo mbali mbali vinavyowakabili wasanii ikiwemo kasi ya mabadiliko ya teknolojia, miundombinu ya sanaa, soko la kazi za sanaa, ambapo sanaa za ndani zinashindwa kuhimili ushindani wa sanaa za nje.

### 2.14 Vijana na Michezo

Michezo ni aina zote za ushughulishaji mwili ambao hupelekea uchangamfu wa mwili, utimamu wa akili na ushirikiano na wengine. Hii hujumuisha michezo midogo midogo, michezo ya mashindano, michezo ya kujifurahisha na michezo ya asili. Michezo inajumuisha harakati zinazohusisha jamii kwa lengo la kuburudisha au kushindana zinazozingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu za Nchi na mashirikisho ya kikanda na Kimataifa . Sekta ya michezo imekuwa ikiwapatia Vijana fursa mbali mbali zikiwemo ajira, kutambulikana na jamii, kulitambulisha Taifa, kujikinga na maradhi mbali mbali, kujikinga na vitendo viovu na kutunza na kudumisha amani na utulivu.

Vijana wamekuwa wakijishughulisha sana na michezo pamoja na kuwepo kwa wanamichezo wenye vipaji na uwezo mkubwa wa kucheza michezo mbali mbali ndani na nje ya Nchi lakini kumekuwepo na vikwazo mbali mbali vinavyowakabili wanamichezo ikiwa ni pamoja na uhaba wa miundombinu ya michezo na vifaa, uhaba wa wafadhili ukosefu wa wataalamu wa fani za michezo pamoja na uhaba wa vyuo na vituo vya michezo.

## SURA YA TATU

## 3.0 DIRA, DHAMIRA, MALENGO MAKHUSUSI NA KANUNI ELEKEZI ZA SERA

### 3.1 Umuhimu wa Kuundwa kwa Sera

Toleo la kwanza la Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar lilichapishwa mwaka 2005 kwa kuzingatia taarifa na mazingira ya wakati huo ikiwa ni pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA). Katika kipindi cha takribani miaka kumi na saba ya utekelezaji wa sera hii kumekuwa na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kimazingira ndani ya Zanzibar na Duniani kwa ujumla. Hii ni pamoja na kuandaliwa kwa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 (Zanzibar Development Vision 2050), Mpango wa Maendeleo Zanzibar 2021-2026 (Zanzibar Development Plan 2021-2026) na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2015-2030 (Sustainable Development Goals 2015-2030) ambayo ni badala ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 na Malengo ya Milenia 2000-2015 (Millenium Development Goals 2000-2015).

Sera ya Maendeleo ya Vijana ya 2005 ni miongoni mwa sera muhimu zilizofanikisha shughuli za maendeleo ya Vijana Nchini. Katika utekelezaji wake, imefanikisha kuratibu na kusimamia shughuli za Vijana, kuundwa kwa Baraza la Vijana kisheria, uanzishwaji wa programu za uwezeshaji Vijana kiuchumi, kushajiisha ushiriki na ushirikishwaji kwa Vijana na kujenga uwezo wa Asasi za kiraia (NGO's) katika maeneo mbali mbali. Pamoja na mafanikio makubwa ya utekelezaji wa sera hiyo, bado ilikuwa na mapungufu mengi ambayo yanakwamisha baadhi ya shughuli za maendeleo ya Vijana. Miongoni mwa mapungufu hayo ni:-

1. Sera haikuweka wazi namna ya kuratibu na kusimamia shughuli za Vijana kwa taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za kiserikali ;

2. Sera imeelekeza kuanzishwa kwa Baraza la Vijana lakini haikuainisha majukumu ya Baraza la Vijana;
3. Sera imetaja stadi za maisha kama ni njia za kukabiliana na tatizo la ajira pekee na kuacha kuzungumzia maswala ya afya na matatizo mengine yaliyomo ndani ya jamii
4. Sera haikufafanua namna ya Vijana kushiriki katika nafasi za maamuzi;
5. Sera haikutambua uvumbuzi na ubunifu wa sayansi na teknolojia pamoja na athari zake;
6. Sera haikufafanua na kuzingatia vya kutosha masuala ya kiutamaduni, maadili, sanaa na michezo; na
7. Sera haikutoa maelezo ya kutosha juu ya ukatili, udhalilishaji na unyanyapaa wa kijinsia na watu wenye ulemavu na mahitaji maalum.

Hivyo, Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya Mwaka 2005 imefanyiwa marekebisho makubwa ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa na ya siku zijazo. Vile vile, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais imeandaa Mwongozo wa Uandaaji na Uandishi wa Sera Zanzibar (toleo la mwaka 2023), maudhui na mtiririko wa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2023 imezingatia maelekezo yaliyomo kwenye mwongozo huo.

### 3.2 Dira ya Sera

Zanzibar yenye Vijana wazalendo, wanaojiamini na kuwa rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

### 3.3 Dhamira ya Sera

Kukuza ustawi na maendeleo ya Vijana kwa kuwajengea mazingira wezeshi na endelevu yatakayoimarisha ushiriki na ushirikishwaji wao katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

### 3.4 Lengo Kuu la Sera

Kuwa na muongozo wa Kitaifa utakaosimamia na kuratibu maendeleo ya Vijana Nchini ili kuwawezesha Vijana kupata fursa na haki zao za msingi za kiuchumi, kijamii na kisiasa

### 3.5 Malengo Mahususi

1. Kuimarisha uratibu. usimamizi, ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa sera na programu za maendeleo ya Vijana Nchini;
2. Kuweka mifumo na mazingira bora itakayowawezesha Vijana kujiajiri na kuajirika;
3. Kukuza uTaifa, utamaduni wa kujitolea, uzalendo, maadili na uwajibikaji miongoni mwa Vijana katika kulitumikia Taifa wakati wowote;
4. Kujenga misingi ya utawala bora, amani, umoja na mshikamano miongoni mwa Vijana na jamii kwa ujumla.
5. Kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha Vijana wenye mahitaji maalum kushiriki na kushirikishwa kikamilifu katika kupanga na utekelezaji wa programu za maendeleo ya Vijana;
6. Kukuza vipaji, uthubutu na uwezo wa Vijana katika nyanja za elimu, sayansi, teknolojia, michezo, utamaduni, sanaa na ubunifu;
7. Kuwajengea uwezo Vijana katika stadi za maisha ili kukabiliana na maradhi , utumiaji wa dawa za kulevya, udhalilishaji, afya ya akili, afya ya uzazi na majanga mengine mbali mbali;
8. Kushajihisha Vijana katika kulinda na kuhifadhi mazingira;
9. Kuhamasisha usawa wa kijinsia na kushiriki vita dhidi ya unyanyasaji na ukatili wa jinsia;
10. Kushajihisha wadau mbali mbali kuandaa miradi, programu, mipango na miongozo ya Kitaifa inayohusu maendeleo ya Vijana katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni;

### 3.6 Kanuni Elekezi za Sera

Kanunu elekezi za sera hii zitatekelezwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ambayo imeainishwa katika majukumu ya Wizara kama ifuatavyo:-

1. *Uzalendo na Uadilifu*: Sera inahimiza Vijana kuweza kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Nchi kwa uzalendo, uadilifu na kujituma zaidi kwa maendeleo yao na Nchi yao;

2. *Usawa na Usawa wa Kijinsia*: Sera inasisitiza usawa wa kijinsia na kupinga udhalilishaji dhidi ya Vijana, Wanawake na watoto. Pia, sera inapiga vita ubaguzi dhidi ya ukabila, itikadi za siasa, dini na eneo mtu analotoka;

3. *Uwajibikaji:* Sera ya Maendeleo ya Vijana inahamasisha uwajibikaji na kufanya kazi kwa bidii ili kuharakisha maendeleo yao na Taifa;

4. *Ushiriki na Ushirikishwaji*: Sera ya Maendeleo ya Vijana inaamini na kuzingatia Vijana ni nguvu kazi ya Taifa. Hivyo ushiriki na ushirikishwaji utaharakisha maendeleo yao na Taifa;

5. *Utawala Bora:* Sera inahimiza misingi ya utawala bora katika maendeleo ya Vijana ili iwe chachu ya kuleta amani, umoja na maendeleo ya Nchi ;

6. *Ubunifu:* Sera inasisitiza masuala ya ubunifu na kuendeleza vipaji kwa Vijana;

7. *Kujitolea:* Sera inahamasisha suala la kujitolea kwa Vijana ili kukuza weledi na utayari katika kazi, kukuza uzalendo na kuharakisha maendeleo ya Nchi ; na

8. *Mtazamo Chanya*: Sera inasisitiza kuwa na mtazamo chanya katika kubaini, kutumia na kunufaika na fursa na maendeleo ya Nchi .

## SURA YA NNE

## 4.0 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA

### 4.1 Hoja ya Sera: Vijana na Afya

Afya ni hali ya kuwa mzima kimwili na kiakili na kuweza kutekeleza majukumu yanayomkabili binaadamu. Afya bora ni miongoni mwa mambo muhimu kwa mustakbali wa Nchi yetu katika kujenga uchumi. Vijana wamo katika hatari ya kukabiliwa na matatizo mbali mbali ya kiafya yakiwemo maradhi ya kujamiana, maradhi ya kisukari, sindikizo la damu, afya ya akili, mimba za umri mdogo.

#### *4.1.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itaimarisha utoaji wa elimu na huduma rafiki ya afya kwa Vijana ili kuimarisha afya zao, kinga na kupambana dhidi ya maradhi mbali mabali yanayowakabili.*

#### *4.1.2 Mikakati ya Sera*

i. Kuendeleza na kuimarisha programu za elimu na huduma ya afya ya uzazi na akili kwa Vijana;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa, elimu na huduma kwa Vijana kujikinga na maradhi yanayoambukiza na yasioambukiza;
iii. Kuimarisha utoaji wa huduma rafiki za afya kwa Vijana;
iv. Kuimarisha elimu na matumizi ya lishe bora kwa Vijana; na
v. Kuimarisha mazingira bora ya kisera, kisheria na Programu zinazohusu upatikanaji wa huduma za afya bora kwa Vijana.

### 4.2 Hoja ya Sera: Vijana na Utawala Bora na Uzalendo

Utawala bora, amani na utulivu ndio msingi wa maendeleo ya Taifa, hivyo Serikali inaamini kwamba uandaaji vyema wa Vijana ndio chachu ya maendeleo ya Taifa na utakaopelekea kuwa na Taifa imara lenye Vijana

wazalendo, waadilifu na kuwa raia wema na viongozi bora ili kuimarisha uwajibikaji na uadilifu wao katika kushiriki kikamilifu katika uimarishaji wa utawala bora na maendeleo Nchini.

#### *4.2.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itawajengea uwezo na mazingira wezeshi na rafiki Vijana ili kupata haki zao za msingi, kujielewa, kuwa wazalendo na kushiriki kikamilifu katika kuimarisha utawala bora Nchini.*

#### *4.2.2 Mikakati ya Sera*

i. Kuimarisha ushiriki wa Vijana katika suala la uimarishaji na utunzaji wa amani na utulivu Nchini;
ii. Kuimarisha programu za kuwaandaa Vijana kuwa na maadili mema, moyo wa uzalendo, uwajibikaji na raia wema kwa Taifa;
iii. Kusimamia na kuziimarisha taasisi, asasi na majukwaa ya Vijana ili kufuata misingi ya utawala bora, uwajibikaji na uwazi;
iv. Kuwaandaa Vijana kufahamu vyema historia ya Nchi yao pamoja na kuwa viongozi bora wa sasa na baadae kwa maslahi ya Taifa;
v. Kuratibu na kushajihisha Vijana wa Zanzibar waliopo nje ya Nchi kuipenda Nchi yao na kuendeleza na kuanzisha jumuiya zao ughaibuni; na
vi. Kuandaa mazingira bora kwa Vijana kupata haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria za Nchi .

### 4.3 Hoja ya Sera: Vijana Ajira na Uwezeshaji kiuchumi

Ukosefu wa ajira kwa Vijana Zanzibar, pamoja na mambo mengine husababishwa na uwezo na uthubutu mdogo wa Vijana, utayari, uweledi wa kujiajiri pamoja na uhaba wa nafasi za ajira kutoka Serikali ni na katika sekta binafsi. Vijana wanaomaliza elimu ya lazima na elimu ya juu wanakabiliwa na changamoto ya ajira.

#### *4.3.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itaandaa mazingira na mipango madhubuti ya kuwawezesha Vijana kujiajiri na kuajiriwa.*

#### *4.3.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kuandaa mazingira bora ya kisera, kisheria na mipango kwa Vijana kushiriki kikamilifu katika uzalishaji mali na utoaji wa huduma;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa na fursa za ajira na uwezeshaji kwa Vijana wote;
iii. Kushirikiana na taasisi za fedha na sekta binafsi kuwawezesha Vijana kupata mitaji ya fedha, mafunzo na masoko kwa bidhaa wanazozalisha;
iv. Kuimarisha ushiriki wa Vijana katika sekta za kiuchumi zikiwemo uchumi wa buluu, biashara, viwanda, kilimo na ufugaji;
v. Kuanzisha na kuimarisha programu maalum za uwezeshaji wa Vijana kimitaji, masoko, mafunzo kazi na usaidizi kazini;
vi. Kuimarisha programu za ajira na ujasiriamali kwa Vijana wa kike na wa kiume pamoja na watu wenye ulemavu na mahitaji maalum; na
vii. Kuimarisha programu za kubadili mtazamo hasi wa Vijana juu ya kujiajiri na kufanya kazi kwa bidii.

### 4.4 Hoja ya Sera: Vijana na Elimu

Sekta ya Elimu ni nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa katika Taifa lolote lile ulimwenguni. Kuna kundi la Vijana ambao hawakupata misingi mizuri ya elimu na kubaki kuwa hawana uwezo wa kujiendeleza na kujiajiri. Serikali katika juhudi zake za kuimarisha nguvu kazi kwa Vijana imekuwa ikitilia mkazo zaidi suala la elimu kwa kuweka juhudi mbali mbali za kuimarisha upatikanaji wake. Pamoja na hayo jitihada kubwa inahitajika kuimarisha mfumo wa elimu ili kumuwezesha kijana kujiajiri na kuajirika kwa mujibu wa mahitaji ya soko la ajira.

#### *4.4.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itaimarisha mfumo wa elimu utakaokidhi mahitaji ya soko la ajira kwa Vijana ndani na nje ya Nchi .*

#### *4.4.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kutoa fursa za masomo na ufadhili kwa Vijana wa kike na wa kiume ndani na nje ya Nchi ;
ii. Kuimarisha ubora wa elimu katika skuli, vyuo na vyuo vikuu ili kuzalisha Vijana wenye sifa za kuajirika au kujiajiri;
iii. Kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa kukuza uwezo wa walimu kitaaluma;
iv. Kuendeleza ushirikiano na wadau wa kuendeleza elimu kwa Vijana wa jinsia zote;
v. Kuimarisha upatikanaji wa fursa na mikopo ya elimu ya juu kwa Vijana; na
vi. Kuhamasisha ufundishwaji wa masomo ya sayansi, hesabu, teknolojia, uhandisi na ubunifu.

### 4.5 Hoja ya Sera: Vijana na Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Amali na Ujasiriamali

Elimu ya ufundi na mafunzo ya amali ni aina ya mafunzo yanayowezesha Vijana kujifunza stadi na maarifa ya kazi na ujasiriamali ili kuweza kujiajiri na kuajirika.

Vyuo na vituo vingi vya elimu ya ufundi na mafunzo ya amali hufundisha bila ya kuzingatia mahitaji tofauti ya wanafunzi, jamii na soko la ajira, hali inayopelekea wahitimu wengi kuchelewa au kushindwa kupata ajira wanapomaliza mafunzo yao. Vyuo na vituo vyetu vina upungufu wa wataalamu, zana na nyenzo za kujifunzia, hali inayopelekea utoaji wa mafunzo usiokidhi mahitaji ya Nchi na soko la ajira.

#### *4.5.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itaimarisha mfumo wa utoajii wa elimu ya ufundi, mafunzo ya amali na ujasiriamali ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi na soko la ajira.*

#### *4.5.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kuimarisha kada ya wakufunzi watakaofundisha walimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali;
ii. Kuwashirikisha mafundi wazoefu wa fani mbali mbali kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali;
iii. Kuimarisha miundombinu na vifaa vya kisasa na rafiki kwa Vijana wa jinsia zote wakiwemo wenye ulemavu na mahitaji maalum kupata mafunzo yatolewayo;
iv. Kuimarisha mitaala ya elimu itakayoendana na mahitaji ya soko la ajira Kitaifa, kikanda na Kimataifa kwa Vijana wa jinsia zote;
v. Kuanzisha na kuendeleza programu maalum za kuimarisha vipaji na ubunifu kwa Vijana; na
vi. Kuendeleza programu za uwezeshwaji wa mitaji,masoko na usimamizi kwa Vijana wa jinsia zote wanaomaliza elimu ya ufundi na mafunzo ya amali na ujasiriamali.

### 4.6 Hoja ya Sera: Vijana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Matumizi ya tekenolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku. TEHAMA inawasaidia Vijana katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa, uwajibikaji, ufanisi, utawala bora na uwazi katika sekta za umma na binafsi.

Vijana ni watumiaji wakubwa na wahanga wa matumizi mabaya ya TEHAMA ikiwemo mmong'onyoko wa maadili, kushiriki katika vitendo viovu vya uvunjifu wa amani ya Nchi , wizi, udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia. Jitihada zinahitajika kuongeza upatikanaji wa taarifa na matumizi sahihi ya teknolojia

kwa Vijana zinazofungua fursa ya Vijana kuwa wabunifu, wazalishaji na kutoa huduma zaidi na zenye ubora kwa jamii.

***4.6.1 Tamko la Sera:***

*Serikali itaimarisha ubunifu wa Vijana na upatikanaji wa taarifa, mafunzo, udhibiti, na matumizi sahihi ya TEHAMA kwa Vijana.*

***4.6.2 Mikakati ya Sera:***

i. Kuimarisha mazingira bora na rafiki ya upatikanaji na matumizi sahihi ya TEHAMA kwa Vijana wa mjini na vijijini;
ii. Kuhamasisha Vijana juu ya matumizi sahihi ya TEHAMA kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla;
iii. Kukuza elimu, mafunzo na ubunifu kwa Vijana kupitia TEHAMA;
iv. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa Wanawake na Vijana wenye ulemavu na mahitaji maalumu; na
v. Kuimarisha matumizi ya vyombo vya habari katika kuelimisha na kuhamasiha maendeleo kwa Vijana.

**4.7 Hoja ya Sera: Vijana Wenye Ulemavu na Wenye Mahitaji Maalum**

Jamii ya Wazanzibari imekuwa na muamko mzuri wa kuwajali, kuwathamini, kuwashirikisha na kuwaendeleza Vijana wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Ili Vijana wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum waweze kushiriki na kushirikishwa katika shughuli mbali mbali za maendeleo, jitihada zaidi zinahitajika za kuelimisha jamiii juu ya kushirikiana nao katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii na kuliletea maendeleo Taifa.

***4.7.1 Tamko la Sera:***

*Serikali itashirikisha Vijana wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum katika shughuli zote za kimaendeleo katika sekta zote.*

*4.7.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kuandaa mazingira bora na rafiki ya kisera na kisheria ili kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum katika maendeleo ya Taifa;
ii. Kuimarisha programu za uwezeshaji kiuchumi kwa Vijana wenye mahitaji maalumu na wenye ulemavu;
iii. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa na mawasiliano kwa Vijana wenye ulemavu na mahitaji maalum; na
iv. Kuweka miundo mbinu bora na wezeshi itakayowawezesha Vijana wenye ulemavu na mahitaji maalum kupata huduma na fursa za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**4.8 Hoja ya Sera: Vijana na Mazingira**

Katika harakati zake za kila siku, mwanadamu huzungukwa na mazingira ambayo ni jumla ya mambo yote ikewemo ardhi, bahari, mito, mimea, wanyama pamoja na sehemu anayoishi. Ushiriki wa Vijana katika uhifadhi, utunzaji na uendelezaji wa mazingira zinasaidia kuimarisha afya za jamii pamoja na kuwa chanzo endelevu cha kuzalisha chakula na ajira zaidi kwa Vijana kupitia matumizi ya taka taka kama malighafi katika uzalishaji wa bidhaa mbali mbali katika biashara na kilimo.

*4.8.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itahakikisha kuwa Vijana wanashiriki ipasavyo katika kulinda na kuhifadhi mazingira Nchini.*

*4.8.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kuhamasisha Vijana wa jinsia zote kuhifadhi na kutunza mazingira katika maeneo wanayoishi na maeneo mengine ya Nchi ;
ii. Kuwezesha na kusimamia Vijana na jamii kutumia rasilimali za bahari, mito, mimea na ardhi kwa mujibu wa miongozo ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira;

iii. Kuhamasisha na kuziwezesha taasisi za Vijana na Vijana wenyewe kushiriki katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa manufaa ya Taifa;
iv. Kuingiza elimu ya mazingira katika elimu na mafunzo ya Vijana;
v. Kutumia vyombo vya habari kusambaza elimu ya mazingira kwa Vijana; na
vi. Kuandaa na kuendeleza program za Mazingira zitakazozalisha Ajira kwa Vijana.

### 4.9 Hoja ya Sera: Ushiriki na Ushirikishwaji wa Vijana

Ushiriki na ushirikishwaji ni mfumo wa jamii unaowezesha kuwa na maamuzi ya pamoja katika kupanga na kutekeleza ili kufikia maendeleo katika jamii. Licha ya juhudi za Serikali katika kutekeleza mipango na maazimio ya ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana, jitahada bado zinaonekana ni ndogo na hazitoi mwanga katika kufikia malengo ya ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika ngazi za maamuzi, kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ya Kitaifa katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

#### *4.9.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itaongeza wigo na fursa za ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana wa makundi yote katika kupanga, kutekeleza kutathmini na kutoa maamuzi ya mipango ya maendeleo ya Taifa.*

#### *4.9.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kujenga mazingira wezeshi ya kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika ngazi mbali mbali za uongozi na maamuzi;
ii. Kulisimamia na kuliimarisha kiutendaji Baraza la Vijana Zanzibar ili kuendelea kuwaunganisha pamoja Vijana bila ya kujali tofauti zao ikiwemo; itikadi za kisiasa, kidini, ukabila na kielimu;
iii. Kuliendeleza na kuliimarisha Baraza la Vijana Zanzibar;

iv. Kuimarisha uwezo wa kiutendaji kwa taasisi na asasi za maendeleo ya Vijana Zanzibar;
v. Kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika kupanga na kutekeleza shuguli za maendeleo yao na Taifa;
vi. Kuandaa miongozo na kuratibu shughuli za maendeleo ya Vijana Zanzibar;
vii. Kuandaa na kuimarisha majukwaa ya ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana kiuchumi, kijamii na kiutamaduni;
viii. Kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana wa Zanzibar katika mambo yanayowahusu Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ; na
ix. Kuandaa na kuimarisha programu za kujitolea kwa Vijana.

### 4.10 Hoja ya Sera: Vijana na Mapambano dhidi ya Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia

Matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya Wanawake na Vijana yamekuwa yakijitokeza na kuongezeka mara kwa mara hapa Zanzibar. Matukio maarufu ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ni pamoja na ubakaji, ndoa za kulazimishwa, unyanyasaji wa kingono, vipigo na kutelekeza familia na mimba katika umri mdogo. Hali hii inaonyesha kuwa matendo ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa Wanawake na Vijana Zanzibar yapo na yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na ufahamu mdogo kati ya Wanawake na Vijana wenyewe na jamii kwa ujumla.

#### *4.10.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itasimamia na kuendeleza programu mbali mbali za kupambana na ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa Vijana wa makundi yote.*

#### *4.10.2 Mikakati ya Sera*

i. Kuhamasisha na kutilia mkazo usawa wa kijinsia kwa maendeleo ya Vijana Zanzibar;

ii. Kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, maazimio na miongozo ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia kwa Vijana;
iii. Kuimarisha mifumo ya uratibu na ufuatiliaji wa mipango ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa Vijana wa makundi yote;
iv. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za hifadhi, ulinzi na marekebisho kwa Vijana wahanga na watendaji wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia; na
v. Kuimarisha programu za uwezeshaji wa Vijana wa kike kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

### 4.11 Hoja ya Sera: Vijana na Utamaduni na Sanaa

Utamaduni, na sanaa ni maeneo ambayo yanapotumiwa vizuri na Vijana husaidia kuwapatia ajira, kuwapatia fedha na umaarufu na kukuza hadhi ya Taifa letu. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha maeneo hayo, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya utamaduni na sanaa na kuweka miongozo ya kisera na kisheria. Hata hivyo Vijana wengi hawajafanya vizuri katika maeneo hayo hasa katika kuitangaza na kuipa hadhi Nchi duniani. Upungufu kwa miundombinu, nyenzo, utaalamu, walimu na programu za utamaduni na sanaa kwa Vijana ni sababu kubwa inayopelekea Vijana kutokufanya vizuri katika maeneo haya.

#### *4.11.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itaendeleza na kuimarisha Sekta za Utamaduni na Sanaa kwa maendeleo ya Vijana na Taifa.*

#### *4.11.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kukuza na kuendeleza utamaduni, mila, silka, desturi zetu na malezi bora kwa Vijana;
ii. Kuendeleza na kuimarisha programu za sanaa na burudani pamoja na kuibua na kuviendeleza vipaji vya Vijana;

iii. Kuwasaidia Vijana wa jinsia zote kushiriki katika mashindano ya sanaa na utamaduni ndani na nje ya Nchi ;
iv. Kuwasaidia Vijana wa jinsia zote kufanya maonyesho ya kazi zao za sanaa na utamaduni;
v. Kutayarisha mipango mahsusi ya kuwezesha burudani na sanaa kuwa ni ajira rasmi ndani na nje ya Nchi ; na
vi. Kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo zitakazowawezesha na kuwahamasisha Vijana wa jinsia zote kushiriki kikamilifu katika shughuli za utamaduni na sanaa.

**4.12 Hoja ya Sera: Vijana na Michezo**

Michezo ni sekta ambayo Vijana wakiitumia vizuri husaidia kuwapatia ajira na kukuza hadhi ya Vijana mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Michezo kama ilivyo sanaa inaongoza kuwapatia fedha na umaarufu Vijana wengi ulimwenguni. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha eneo hili, ikiwemo ujenzi na kuimarisha miundombinu ya michezo iliyopo. Hata hivyo Vijana hawajafaidika vya kutosha katika eneo hili la michezo. Hii inatokana na uhaba kwa miundombinu, vifaa na utaalamu, motisha na hamasa ya michezo kwa Vijana.

***4.12.1 Tamko la Sera:***

*Serikali itaendeleza na kuimarisha Sekta ya Michezo kwa maendeleo ya Vijana na Taifa.*

***4.12.2 Mikakati ya Sera:***

i. Kuendeleza na kuimarisha programu mbali mbali za michezo kwa Vijana wa kike na kiume;
ii. Kuwasidia Vijana wa jinsia na hali zote kushiriki katika mashindano ya michezo ndani na nje ya Nchi ;
iii. Kuendeleza na kuimarisha elimu na mafunzo ya michezo kwa Vijana wa jinsia zote;

iv. Kutayarisha mpango mahsusi wa “michezo na ajira kwa Vijana;
v. Kuimarisha miundombinu ya michezo kwa kila Wilaya;
vi. Kuwahamasisha Vijana wa jinsia zote kushiriki kikamilifu katika shughuli za michezo; na
vii. Kuanzisha vituo na akademia za michezo kwa lengo la kukuza, kulea na kuendeleza vipaji vya Vijana wa jinsia na hali zote.

### 4.13 Hoja ya Sera: Vijana na Stadi za Maisha

Mafunzo ya stadi za maisha kwa Vijana ni jambo la msingi katika kumuandaa kijana kujitambua na kuweza kukabiliana na mabadiliko ya kimwili na kiakili ili kuepukana na vitendo vitakavyohatarisha afya na maendeleo yake binafsi. Stadi za Maisha pia humsaidia kijana kuweza kufanya maamuzi sahihi, kukabiliana na shindikizo rika, maradhi yasiyoambukiza na yanayoambukiza, dawa za kulevya, udhalilishaji wa kijinsia na kuweka malengo na kusimamia ufanikishaji wa malengo yake

#### *4.13.1 Tamko la Sera:*

*Serikali itaweka mazingira bora na rafiki ya upatikaji wa mafunzo ya stadi za maisha kwa Vijana walio ndani na nje ya skuli.*

#### *4.13.2 Mikakati ya Sera:*

i. Kuweka na kutekeleza miongozo na mipango maalum itakayowashirikisha wadau katika uimarishaji wa mafunzo ya stadi za maisha kwa Vijana;
ii. Kuandaa na kuendeleza mafunzo ya stadi za maisha kwa Vijana;
iii. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa utoaji wa mafunzo wa stadi za maisha kwa Vijana yanayoendana na mila, silka na utamaduni wa mzanzibari;
iv. Kuanzisha na kuendeleza vituo vya mafunzo na maendeleo ya Vijana; na
v. Kuimarisha program za kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya, UKIMWI, afya ya akili, mimba za umri mdogo, ndoa za mapema na mporomoko wa maadili.

**SURA YA TANO**

# 5.0 MFUMO WA KITAASISI, KISHERIA NA URATIBU WA SERA

## 5.1 Mfumo wa kitaasisi na uratibu

Wizara kupitia Idara inayosimamia maendeleo ya Vijana itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera hii. Katika kufanikisha hilo, Wizara itaandaa na kusimamia Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ili kuhakikisha kila mhusika anatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi na kuhakikisha lengo la sera linafikiwa.

## 5.2 Mfumo wa kisheria

Kutakuwa na mfumo wa uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera hii utakaosimamiwa na Wizara yenye dhamana ya Vijana kupitia Idara husika na kushirikisha sekta mbali mbali za Serikali na zisizo za kiserikali ili kutathmini utekelezaji wa sera hii na kupata ripoti halisi za utekelezaji zitakazowasilishwa kwa mamlaka husika pamoja na wadau mbali mbali wa maendeleo ya Vijana. Wizara pia itazihamasisha taasisi za Serikali na wahusika wengine kuzingatia na kuingiza masuala ya maendeleo ya Vijana ndani ya sera, mipango, programu, miradi na shughuli za taasisi zao.

## 5.3 Majukumu na wajibu wa wadau katika utekelezaji wa Sera

Katika kuhakikisha utekelezaji wa sera hii unakuwa shirikishi na wenye ufanisi mkubwa, sera imeainisha wadau mbali mbali na majukumu yao ya utekelezaji ili waweze kuzingatia katika mipango yao na kuchukua hatua za utekelezaji katika kufikia lengo la Sera hii. Wadau na majukumu yao ni kama yafutayo:

### *5.3.1 Wizara Inayohusika na Masuala ya Maendeleo ya Vijana*

i. Kupanga, kusimamia na kuratibu mipango ya utekelezaji wa sera na maendeleo ya Vijana Nchini;

ii. Kuimarisha ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za maendeleo ya Vijana;
iii. Kuhakikisha kuwa masuala ya Vijana yanazingatiwa katika Sera, mipango, programu na miradi ya kisekta na Kitaifa;
iv. Kuhakikisha kuwa sheria zinazohusiana na utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana zinatungwa, kufanyiwa mapitio na kutekelezwa kwa ukamilifu;
v. Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa rasilimali na nyenzo kwa ajili ya utekelezaji wa sera, mipango, programu na miradi ya maendeleo ya Vijana;
vi. Kusimamia na kuratibu utendaji wa Baraza la Vijana Zanzibar kwa mujibu wa sera na sheria za Nchi ; na
vii. Kuzijengea uwezo taasisi na wadau wa maendeleo ya Vijana.

### *5.3.2 Wizara inayohusika na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali*

i. Kuratibu na kutoa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali na miongozo juu ya matumizi sahihi ya teknolojia kwa Vijana;
ii. Kujenga na kuimarisha vyuo vya ufundi na mafunzo ya amali na kutoa mafunzo kwa Vijana;
iii. Kuhakikisha kuwa Vijana wanapatiwa taaluma za ufundi, biashara na stadi za uongozi katika fani mbali mbali zinazokidhi mahitaji ya soko la ajira;
iv. Kuendeleza mfuko maalum kwa Vijana wanaomaliza elimu ya ufundi na mafunzo ya amali; na
v. Kukuza taaluma za sayansi na teknolojia ili kukuza ueledi, ubunifu na vipaji kwa Vijana.

### *5.3.3 Wizara inayohusika na Elimu*

i. Kuongeza fursa ya elimu ya juu kwa Vijana;
ii. Kuhakikisha kuwa mikopo ya elimu ya juu inatolewa kwa Vijana wote

wenye sifa;

iii. Kuwarejesha na kuwapatia elimu mbadala wanafunzi walioacha masomo;
iv. Kuimarisha elimu ya uzalendo, utawala bora na maadili ndani ya mfumo wa elimu; na
v. Kupitia na kuandaa mitaala ya elimu itakayowaandaa Vijana kupata ajira na kuwa weledi na mahiri.

### *5.3.4 Wizara inayohusika na Ajira, Kazi na Utumishi wa Umma*

i. Kuandaa sera na mipango madhubuti ya kuimarisha fursa za ajira kwa Vijana;
ii. Kujenga mazingira bora ya kazi kwa Vijana kujiajiri na kuajiriwa ndani na nje ya Zanzibar;
iii. Kuanzisha na kuviimarisha vituo vya kutoa taarifa za soko la ajira kwa Vijana wanaotafuta kazi;
iv. Kuimarisha udhitibiti wa utoaji wa vibali vya kazi kwa wageni; na
v. Kusimamia sheria za kazi, ikiwemo afya na usalama kazini na ustawi wa Vijana kwenye sekta zote za ajira.

### *5.3.5 Wizara inayohusika na Habari na Mawasiliano*

i. Kuhakikisha kuwa vituo vya elimu ya habari na mawasiliano vinaanzishwa na kuimarishwa;
ii. Kutoa taarifa na elimu juu ya maendeleo na ustawi wa Vijana;
iii. Kuwaunganisha Vijana na fursa za ajira zilizopo kwa wawekezaji wa ndani na nje; na
iv. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa na matumizi sahihi ya technolojia ya habari na mawasiliano

### *5.3.6 Wizara inayohusika na Utalii na Uchumi wa Buluu*

i. Kuelimisha juu ya biashara ya utalii na kujenga mazingira mazuri yatakayowawezesha Vijana kuwekeza katika sekta hiyo;

ii. Kuandaa na kuratibu ushiriki wa Vijana katika sekta za utalii na uchumi wa buluu pamoja na matamasha mbali mbali ya utalii ndani na nje ya Nchi ;
iii. Kuhamasisha mamlaka ziliopo kusimamia zaidi upatikanaji wa fursa za ajira katika sekta ya utalii vijijini; na
iv. Kuwaelimisha na kuwawezesha Vijana kuwekeza na kushiriki kikamilifu katika kukuza na kuendeleza dhana ya uchumi wa buluu.

### *5.3.7 Wizara inayohusika na Kilimo, Maliasili na Mifugo*

i. Kuimarisha sekta ya kilimo, ufugaji na mali ya asili ili iwe rafiki na kutengeneza ajira zaidi kwa Vijana;
ii. Kuwaelimisha na kuwawezesha Vijana kushiriki kikamilifu katika kukuza na kuendeleze maliasili, kilimo na ufugaji;
iii. Kutoa miongozo ya kitaalamu na uwezeshaji wa Vijana juu ya kazi zinazohusiana na, ufugaji, kilimo, uhifadhi na usarifu wa mazao;
iv. Kuelimisha Vijana juu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira na utumiaji mzuri wa maliasili za Nchi kwa maslahi yao na vizazi vijavyo;
v. Kuanzisha mashamba ya mfano na kutoa taaluma kwa Vijana; na
vi. Kuandaa maonyesho ya sekta husika na kuwashirikisha Vijana kuonesha na kuuza bidhaa zao.

### *5.3.8 Wizara inayohusika na Viwanda na Biashara*

i. Kutoa miongozo juu ya sera za Serikali , sheria na kanuni zinazohusu biashara, masoko na uanzishaji na uendelezaji wa viwanda kwa Vijana;
ii. Kuwajengea uwezo Vijana kuanzisha, kumiliki na kuendesha viwanda vidogo na vya kati;
iii. Kuwaelimisha Vijana juu ya utawala na uendeshaji wa biashara na umuhimu wa uzalishaji na utoaji wa huduma zenye viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa ;

iv. Kushajihisha wazalendo na wageni kuwekeza katika sekta ya viwanda na biashara;
v. Kuainisha maeneo ya kufanya biashara kwa Vijana; na
vi. Kusaidia maendeleo ya viwanda na biashara kwa kutoa mikopo nafuu kwa Vijana.

### *5.3.9 Wizara inayohusika na Fedha na Uwezeshaji Kiuchumi*

i. Kuimarisha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa miradi na programu za maendeleo na ustawi wa Vijana Zanzibar;
ii. Kuhakikisha vipaumbele vya Vijana vinazingatiwa katika mipango, mikakati na bajeti kuu ya Serikali ;
iii. Kuhamasisha taasisi za fedha kuweka kipaumbele katika miradi ya maendeleo ya Vijana;
iv. Kutoa mitaji midogo na mikubwa kwa ajili ya uwekezaji katika miradi yenye tija kwa maendeleo ya Vijana;
v. Kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa Vijana kubuni, kuanzisha na kutekeleza miradi yao ya kiuchumi ili waweze kujiajiri na kuajiri wenzao;
vi. Kurekebisha mifumo ya utozaji kodi na kupunguza msururu wa kodi kwa Vijana wanaofanya biashara; na
vii. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu na taarifa za maendeleo na ustawi wa Vijana Nchini.

### *5.3.10 Wizara inayohusika na Sheria na Utawala Bora*

i. Kuweka mifumo mizuri ya mawasiliano na mashirikiano miongoni mwa wadau ili kufikia uwajibikiaji na utawala bora;
ii. Kutunga sheria rafiki kwa maendeleo ya Vijana na kusimamia utekelezaji wake;
iii. Kutoa miongozo na mafunzo kwa Vijana kuhusu utawala bora; na
iv. Kusimamia na kuratibu masuala ya ushiriki na ushirikishwaji wa makundi mbali mbali ya Vijana katika shughuli za maendeleo Nchini.

### *5.3.11 Wizara inayohusika na Afya*

i. Kuandaa mazingira mazuri yatakayowawezesha Vijana kupata taarifa, elimu na huduma za afya ikiwemo haki ya afya ya uzazi;
ii. Kuratibu na kusimamia mipango ya marekebisho ya tabia kwa Vijana walioathirika na wanaotumia dawa ya kulevya; na
iii. Kuhakikisha kuwa mahitaji ya msingi ya afya yanapatika kwa Vijana.

### *5.3.12 Wizara inayohusika na Mazingira*

i. Kuelimisha Vijana juu ya umuhimu wao kushiriki katika kuhifadhi na kutunza mazingira na utumiaji mzuri wa maliasili za Nchi ;
ii. Kuhakikisha Vijana wanajikita kwenye matumizi bora na endelevu ya rasilimali za Nchi ; na
iii. Kuhakikisha kuwa shughuli za kiuchumi na uzalishaji Nchini zinazingatia suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira kisera na kiutendaji.

### *5.3.13 Wizara inayohusika na Mila, Utamaduni na Sanaa*

i. Kuhakikisha kuwa Vijana wanalinda utamaduni, mila, silka na maadili ya Nchi yao kuzuwia athari za utandawazi;
ii. Kuhakikisha kwamba Vijana wanapatiwa elimu sahihi itakayokidhi haja ya kuelewa mila na utamaduni wao;
iii. Kuendeleza sekta ya sanaa na burudani ili kuongeza fursa ya ajira kwa Vijana;
iv. Kusimamia nidhamu katika sanaa na burudani; na
v. Kulinda haki na kubaini fursa kwa wasanii miongoni mwa wadau ndani na nje ya Nchi .

### *5.3.14 Wizara inayohusika na Michezo*

i. Kuhakikisha kuwa Vijana wanashiriki kikamilifu katika michezo ya ndani na nje;
ii. Kuhakikisha Vijana wanapatiwa elimu sahihi ya michezo na elimu kwa

michezo;

iii. Kuendeleza sekta ya michezo kwa Vijana ili kuongeza fursa za ajira kwa Vijana;
iv. Kusimamia nidhamu kwenye michezo na kutunza miundombinu ya michezo;
v. Kulinda haki za Vijana wanamichezo; na
vi. Kuendeleza programu za maendeleo ya michezo kwa Vijana ikiwemo kuibua, kulea na kuendeleza vipaji vya michezo kwa Vijana.

### *5.3.15 Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

i. Kuratibu ushiriki wa Vijana wa jinsia zote katika shughuli za kujitolea na ujenzi wa Taifa;
ii. Kuwaandaa Vijana wa kike na wa kiume kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbali mbali katika maeneo yao na maeneo mengine ya Nchi ; na
iii. Kuimarisha ushiriki wa Vijana katika Serikali za Mitaa.

### *5.3.16 Sekta Binafsi*

i. Kuhakikisha kwamba sekta binafsi inawaendeleza Vijana kitaaluma katika harakati za maisha yao;
ii. Kuzingatia mahitaji ya Vijana katika mipango ya ajira, masoko na ujasiriamali;
iii. Kusaidia Vijana kitaaluma na ushauri kwa kuifikia mitaji na fursa za kujiendeleza kupitia wajibu wa taasisi za binafsi kwa jamii; na
iv. Kutoa ajira na mikopo nafuu kwa Vijana na kutoa fursa za kupatiwa mafunzo kazini.

### *5.3.17 Washirika wa Maendeleo*

i. Kuendelea kusaidia na kuunga mkono juhudi za Serikali na wadau wa maendeleo ya Vijana katika kutekeleza sera, programu na mipango mbali mbali zinazohusiana na maendeleo ya Vijana Nchini; na
ii. Kutoa msaada wa kiufundi na kusaidia upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya Vijana;

iii. Kusaidia kuzijengea uwezo taasisi za maendeleo ya Vijana ili ziweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na weledi zaidi.

#### *5.3.18 Baraza la Vijana Zanzibar*

i. Kuwajenga Vijana kuutambua uTaifa wao, hali ya umoja, uzalendo, mshikamano, kujiheshimu na pia kuifahamu kwa kina jamii, kiuchumi na kiutamaduni;
ii. Kuwawezesha Vijana kutambua umuhimu na wajibu wao kwa jamii;
iii. Kusaidia na kuwaunganisha Vijana na fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii;
iv. Kufanya kazi kama jukwaa na kiungo wakilishi kwa masuala ya Vijana Zanzibar;
v. Kuwakilisha maslahi ya Vijana ndani na nje ya Nchi ;
vi. Kuwajenga Vijana kuwa wazalendo, hali ya umoja, mshikamano, kulinda amani, kujiheshimu na pia kuifahamu jamii kwa kina kiuchumi na kijamii; na
vii. Kukuza mashirikiano na taasisi nyengine zinazoshughulikia maendeleo ya Vijana Nchini.

#### *5.3.19 Asasi za Kiraia*

i. Kuandaa mipango na mikakati ya kusaidia utekelezaji wa sera;
ii. Kufanya ushawishi na utetezi wa masuala ya maendeleo na ustawi wa Vijana;
iii. Kuandaa programu na miradi itakayosaidia utekelezaji wa sera;
iv. Kuhamasisha na kusaidia maendeleo ya Vijana Nchini kwa kutoa taaluma, ruzuku, mikopo na misaada mengine ya kimaendeleo;
v. Kufanya kazi bega kwa bega na Serikali , Baraza la Vijana na wadau wengine wa maendeleo kwa maslahi ya Vijana; na
vi. Kuunga mkono Serikali katika kuimarisha amani, umoja na mshikamano kwa Vijana na Taifa kwa ujumla.

#### *5.3.20 Asasi za Kidini*

i. Kutoa mafunzo na malezi ya kiimani na kiroho kwa Vijana ili wawe raia wema na viongozi bora;
ii. Kupinga vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia kwa Vijana katika jamii;
iii. Kuwafundisha Vijana maadili mema na kuwakataza mabaya ikiwemo kujiunga na makundi maovu na itikadi kali ndani na nje ya Nchi ;
iv. Kuhubiri umoja, amani na mshikamano miongoni mwa Vijana na jamii;
v. Kuhamasisha heshima na uvumilivu wa kidini miongoni mwa Vijana na Jamii;
vi. Kuiunga mkono Serikali katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya Vijana Nchini; na
vii. Kuendeleza na kuimarisha mafunzo ya ndoa na malezi kwa Vijana

#### *5.3.21 Vyombo vya Habari*

i. Kuelimisha na kuhamasisha umma juu ya maendeleo ya Vijana;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa kwa Vijana;
iii. Kutoa elimu na maarifa ili kukuza ushiriki wa Vijana katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni;
iv. Kuibua na kuviunga mkono vipaji vya Vijana ili kukuza kipato na ajira kwa Vijana;
v. Kutoa elimu na mafunzo kwa Vijana ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili; na
vi. Kutambua na kuonesha mchango wa Vijana katika maendeleo ya Taifa.

#### *5.3.22 Jamii na Wazazi*

i. Kuimarisha malezi na makuzi ya Vijana kiuchumi, kijamii na kiutamaduni;
ii. Kuimarisha ukaribu na mawasiliano na Vijana na kuwashirikisha katika mambo yanayowahusu;
iii. Kuwaelimisha Vijana umuhimu wa kufuata mila, silka na utamaduni wa mzanzibari;

iv. Kuimarisha mahusiano ya kindoa na familia ili kuimarisha familia, malezi na ustawi wa Vijana;
v. Kuwashirikisha Vijana katika mgawanyo wa rasilimali katika ngazi ya familia ili kuwajengea uwezo wao wa kiuchumi; na
vi. Kuwaunga mkono na kuwaongoza Vijana katika kufikia maendeleo yao.

### *5.3.23 Vijana*

i. Kujifunza na kuheshimu katiba, sheria, sera, mipango na mikakati ya Nchi ;
ii. Kushiriki katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kufuatilia programu za maendeleo ya Vijana;
iii. Kuwa wazalendo na kushiriki kikamilifu katika shughuli za Maendeleo na ujenzi wa Taifa;
iv. Kujifunza na kuenzi mila, silka na utamaduni wa mzanzibari;
v. Kushiriki kikamilifu katika kuimarisha amani, umoja na mshikamano Nchini;
vi. Kushiriki na kutunza maendeleo na rasilimali za Nchi ;
vii. Kushiriki katika utunzaji, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira;
viii. Kushiriki, kujitolea na kujituma katika shughuli za maendeleo yao na Taifa; na
ix. Kushiriki katika kupinga vitendo viovu ikiwemo; biashara na matumizi ya dawa za kulevya, rushwa na udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia.

**SURA YA SITA**

# 6.0 URATIBU, UFUATILIAJI, TATHMINI NA MAPITIO YA SERA

## *6.1 Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini*

Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana itaandaa mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar. Uratibu, ufuatiliaji na tathmini utafanyika kwa kuzingatia mpango wa utekelezaji wa sera hii na kuwashirikisha wadau wa maendeleo ya Vijana Zanzibar kila robo mwaka na ripoti itajadiliwa katika vikao vya uratibu katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa.

Ripoti hizo za uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya sera ya maendeleo ya Vijana Zanzibar itatoa hali halisi ya utekelezaji wa sera kwa jamii na wahusika mbali mbali kufuatana na Mpango wa Utekelezaji wa sera ulioandaliwa. Changamoto na mapendekezo ya kuimarisha utekelezaji zitajadiliwa na kufanyiwa kazi.

## *6.2 Mapitio ya Sera*

Sera ya Maendeleo ya Vijana itafanyiwa mapitio kila baada ya kupita miaka mitano au pale itakapoonekana kuna haja kutokana na mabadiliko ya sheria, mipango ya maendeleo ya Nchi , sera za Nchi , maendeleo ya Vijana ulimwenguni na kupitishwa na kuridhiwa kwa maazimio mapya yanayohusu ustawi na maendeleo ya Vijana.

## *6.3 Mpango wa Rasilimali wa Sera*

Suala la Vijana ni sulala mtambuka, Hivyo mpango wa Rasilimali fedha utakaokwenda sambamba na mpango wa utekelezaji wa sera na mpango wa ufuatiliaji na tathmini utaandaliwa. Mpango utabainisha rasilimali zitakazohitajika katika utekelezaji wa kila mkakati. Rasilimali fedha kutoka

kwa wadau wote wa maendeleo ya Vijana zikiwemo taasisi za Serikali , asasi za kiraia, washirika wa maendeleo, jamii na Vijana wenyewe zitatumika katika utekelezaji wa sera hii.

Aidha Rasilimali fedha kutoka kwenye bajeti kuu ya Serikali itatumika kwa ajili ya kutekeleza sera hii na kukidhi gharama zinazohitajika ikiwemo kutoa elimu na mafunzo, ajira, vifaa na zana kufanyia kazi, miundombinu, majengo na gharama nyengine zinazohitajika kuwezesha sera hii mpya kutekelezeka kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.

Wadau wa Maendeleo ya Vijana pia wataweza kushiriki kutafuta rasilimali hizo kwa kuandaa miradi na program zitakazowashirikisha washirika wa kimaendeleo kutekeleza sera hii.

### *6.4 Mkakati wa Mawasiliano*

Mkakati wa Mawasiliano wa Sera ya Maendeleo ya Vijana utaandaliwa ili kueleza namna ya elimu ya sera hii itakavyosambazwa kwa wadau kupitia mifumo mbali mbali ya upashanaji wa taarifa. Ufanisi katika mawasiliano utaimarisha na kuongeza ufanisi na msaada wa utekelezaji wa sera. Mawasiliano yataimarisha mshikamano mkubwa baina ya Serikali , Asasi za kiraia, washirika wa kimaendeleo, jamii na Vijana wenyewe. Mkakati wa mawasiliano utarahisisha kutambulika kwa haraka sera hii, Dira, Lengo na Mikakati ya Sera. Aidha, utatambulisha majukumu ya kila mdau. Mkakati wa mawasiliano utaandaa nyenzo za mawasiliano na vipeperushi kwa ajili ya kusambazwa kupitia njia na teknolojia mbali mbali za habari na mawasiliano ili kufikia makundi mbali mbali yakiwemo watu wenye ulemavu.